# Nipashe

Jumatano Februari 23, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580865
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

SportPesa
TZS. 961,840,460
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#




**ACT** 'yanunua' kesi ya makada wa CHADEMA waliofungwa

UKURASA 3




**DE GEA: NAWEZA KUSTAAFIA UNITED**

UKURASA 22



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Askofu wa Jimbo Katoliki la Rulenge wilayani Ngara Mkoa wa Kagera, Severine Niwemugizi, baada ya kuwasili katika viwanja vya Posta Ngara kwa ajili ya kuhudhuria Sherehe za Jubilee ya Miaka 25 ya Utumishi wake wa Kiaskofu(1997-2022), jana. **PICHA: IKULU**

# Rais Samia: Sitaki kuwa Rais wa kutukuzwa

• **Akoleza** moto kukomesha matukio mauaji, awatwisha zigo viongozi wa dini... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

**USHIRIKA WAJITOSA HAMASA CHANJO UVIKO-19**

VIONGOZI wa Bodi ya Chama cha M singi cha Ushirika umoja cha mjini Liwale, mkoani Lindi, kimejitosa kwenye...

## Kamati ya Bunge yamulika usalama bandari

UKURASA 3



UKURASA 2

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Biashara wa Benki ya NMB, Alex Mgeni, alipotembelea Banda la NMB, wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini, jijini Dar es Salaam. Benki hiyo, ikiwa ni moja ya wadhamini wa mkutano huo ulioleta wadau kujadili fursa za uwekezaji nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wawekezaji waonywa uchafuzi mazingira, ajira watoto madini

**MICHEZO** **TFF YASHUKIA WAAMUZI LIGI KUU** UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Saad Mtambule (wa pili kushoto), akikabidhi miche ya miti kwa mmoja wa wananchi wa kijiji cha Ilundi, wilayani humo, mkoani Iringa jana, baada ya kuzindua ugawaji miti kwa taasisi za serikali, wananchi na watu binafsi wanaozunguka shamba la miti la Sao Hill. Habari Uk. 10: **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Samia: Sitakuwa Rais wa kutukuzwa

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kwenye uongozi wake hatakuwa kiongozi wa kutukuzwa licha ya kwamba ndiye mwenye mamlaka ya juu ya uongozi kuliko yeyote nchini.

Amesisitiza kuwa tabia ya kutukuzwa kwa viongozi wanapokuwa madarakani haipendezi kwenye mamlaka, akisema anamwomba Mungu na atajitahidi kutofanya hivyo.

Rais Samia alitoa kauli hiyo jana wakati wa sherehe ya Jubilei ya Miaka 25 ya Mhashamu Askofu Severine Niwemugizi wa Jimbo Katoliki Rulenge iliyofanyika viwanja vya Posta Ngara mkoani Kagera.

"Baba askofu katika hotuba yako umesema nikatae kutukuzwa, nami nikuahidi mbele ya umma huu kwamba hiyo si tabia yangu na ninajitahidi kujishusha, niwe sawa na wengine. Maana utumishi huu ni mipango ya Mungu kuniweka hapa niwatumikie.

"Nitajitahidi kuwa na hekima na uvumilivu na sikio la kusikiliza pia wengine. Nimefurahishwa na kauli ya askofu kwamba 'ninyi ni sauti ya Mungu, mtumike vyema'.

"Ninashukuru kwa hilo ila sauti zetu zitumike kuona watu wanapokengeuka na iwapo watu hawaishi maisha yasiyompendeza Mungu, tuseme," Rais Samia alisema.

**SHIDA YA MAUAJI**

Rais Samia pia alizungumzia matukio ya mauaji ya watu nchini, akisema zinahitajika jitihada za pamoja kuhakikisha yanakomeshwa kwenye jamii.

Alisema jitihada hizo zinapaswa kuanzia shuleni kwa wanafunzi kupewa mafunzo ya maadili na kufahamu utu wa binadamu ili kuwajenga kutojihusisha na matukio ya mauaji.

"Serikali kwa pamoja tunalaani matukio ya mauji na ukatili wa kijinsia, endeleeni kuonya, Mungu anachukizwa na hayo.

"Serikali tutaendelea kutafuta suluhu ya matukio hayo. Lengo letu ni kufanya kazi karibu nanyi (viongozi wa dini), mwonyeshe upungufu na tufanye nini.

"Kama ni kurekebisha sheria na sera zetu tutaona. Nchi hii haiendeshwi na mtu mmoja, kila mmoja achangie, hii itasababisha nchi kuwa na utulivu na amani.

"Matukio ya mauaji na kujiua yanaongezeka na zipo sababu tofauti za matukio haya. Uchunguzi umekuwa ukibaini wivu wa mapenzi, ushirikina, lakini sababu zote hizo zinazobainishwa zinatokana na watu kutokuwa karibu na Mungu. Anayetoa uhai ni Mungu na Mungu ndiye anayeutwaa uhai.

"Mtu anayejali utu wa mwenzke hawezi kufanya haya. Kuna kazi ya kufanya ili kukabiliana na hili, kuwarejesha watu katika imani ya Mungu, viongozi wa dini kurejea mafunzo kwa waumini wao, ili kuwakumbusha mila na dini kwamba haziruhusu mauaji," alisema.

Rais Samia alisema wakati madini ya nickel yakitarajiwa kuanza kuchimbwa huko Ngara kwa ubia, serikali itahakikisha wananchi wananufaika na mradi huo.

**KAULI YA ASKOFU**

Awali Askofu Niwemugizi alisema wataendelea kushirikiana na serikali kwa kuhakikisha kunakuwapo haki na amani nchini.

Kiongozi huyo wa kiroho pia alimwomba Rais Samia kulisaidia kanisa kurejeshewa eneo alilodai limepokwa na halmashauri, akibainisha kuwa walikuwa wanalimiliki kisheria tangu mwaka 1972.

Pia aliomba kanisa kusamehewa deni wanalodaiwa na Mamlaka ya Mapato (TRA) la takribani Sh. milioni 300 kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015.

"Tuna hospitali mbili na zahanati katika jimbo ninaloliongoza. Hospitali teule ya Wilaya na Rulenge, zinahudumia watu maskini sana, kuna wakati wanashindwa hata kulipia huduma, hospitali hatufanyi biashara.

"Tunaomba madeni tuliyonayo ya TRA tusamehewe toka mwaka 2015 Hospitali ya Biharamulo inadaiwa Sh. milioni 113 na Rulenge inadaiwa 213.

"Ngara ina shida ya maji, kwenye mkutano mwaka 2017 Hayati Rais John Magufuli aliahidi kutoa pesa kutoka chanzo Mto Kagera hadi kwenye tangi, tumwombe Rais atusaidie mradi utekelezwe shida ya maji iishe," alisema.

Askofu huyo pia alitumia nafasi hiyo kuwasilisha kilio cha wakulima walioko jimboni kwake, akiiomba serikali kupata masoko ya mazao yao ambayo kwa sasa yananunuliwa kwa bei ndogo.

Askofu Niwemugizi alisema ipo haja ya kutafuta chanzo cha mauaji yanayoendelea kuripotiwa kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Alibainisha kuwa viongozi wa kanisa mkoani Kagera wanatarajia kukutana Machi mwaka huu kujadili suala hilo.

"Uhai ni zawadi ya Mungu, ni Mungu tu ana haki ya kuutoa. Tunahitaji mjadala wa kitaifa kutafakari sababu ni nini. Imefika mahali inaonekana maisha ni tunu na kulindwa kwa gharama yoyote.

"Mtu anaona ni rahisi kuua au kujiua, kuna kosa mahali fulani. Dini kutofundishwa ipasavyo shuleni na vyuoni ni tatizo," alionya askofu huyo.

Aliwataka viongozi wenzake wa dini kupaza sauti kuwakemea watu wote dhidi ya vitendo hivyo.

"Sisi tunalaani matukio ya mauaji na matendo yote ya ukatili, lazima tuonye, Mungu atachukizwa, viongozi wa dini tutaamsha ghadhabu ya Mungu kwa kutokusema, lazima tuonye," alisema.

Alisema amekuwa akifanya kazi hiyo kwa miaka 25 na amekumbana na vikwazo kadhaa katika huduma hiyo na ana imani ataendelea kufanya vyema.

## Serikali yawaonya wawekezaji uchafuzi mazingira, ajira watoto

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imeagiza mambo sita kwa wawekezaji katika sekta ya madini nchini, ikiwamo kuzingatia uhifadhi wa mazingira na kutojihusisha na ajira za watoto migodini.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alitoa maagizo hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa kimataifa wa uwekezaji katika sekta ya madini Tanzania 2022.

Mkutano huo ambao umebebwa na kaulimbiu 'Mazingira Wezeshi kwa Maendeleo ya Sekta ya Madini Tanzania', uliwakutanisha wadau wa sekta hiyo wa ndani na nje ya nchi.

Akizungumza katika mkutano huo wa siku mbili, Dk. Mpango aliyataja mambo mengine ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi na sekta hiyo kuwa ni wawekezaji wenye ubia na serikali waharakishe utekelezaji kwa mujibu wa makubaliano ili wananchi waanze kunufaika.

"Suala la uharibifu wa mazingira, ninawakumbusha wachimbaji wote wakubwa na wadogo kuzingatia sheria za mazingira, wawekezaji wote mna wajibu wa kuhakikisha shughuli zenu za uchimbaji, uchenjuaji na uchakataji wa madini zinatekelezwa kwa mujibu wa sheria na taratibu," alisema.

Dk. Mpango aliwataka wawekezaji wote, hususani wakubwa, wazingatie matakwa yanayotokana na tathmini ya athari kwa mazingira na jamii kwa kuzingatia misingi ya uzalishaji endelevu, matumizi na mbinu bora za uzalishaji wa teknolojia bora na rafiki kwa mazingira.

"Serikali inawaasa wawekezaji pamoja na wachimbaji kutojihusisha na ajira za watoto badala yake mwongeze juhudi za kuhamasisha kukuza uelewa na uwezo wa jamii kwa wachimbaji wadogo hususani wanawake kwa kupitia wataalamu.

"Jambo la tano, tunazikumbusha kampuni zote zinazowekeza kwenye sekta hii, zihakikishe zinatekeleza ipasavyo matakwa ya kisheria ya kuandaa mipango ya ufungaji migodi na kuweka hati fungani ya urekebishaji wa mazingira," alisema

Jambo la sita alizitaka benki na taasisi zingine za fedha kwa kushirikiana na Shirika la Madini (STAMICO) kubuni namna bora zaidi ya kuwawezesha wachimbaji wadogo wakati serikali ikiendelea kulifanyia kazi suala la kuanzishwa kwa benki maalumu ya madini.

"Muendelee kuimarisha uchumi wa wananchi wanaozunguka migodi kwa kutoa fursa za ajira kwa wenyeji na kujenga urafiki na jamii zinazowazunguka ili kuepuka migogoro," aliagiza.

Pia aliitaka Wizara ya Madini iwasilishe taarifa na mapendekezo yatakayotolewa kwenye mkutano huo haraka iwezekanavyo.

"Changamoto zilizosemwa hapa ninazipokea kwa niaba ya Mheshimiwa Rais kama Mheshimiwa Waziri wa Madini alivyosema tutazifanyia kazi.

"Kuhusu kodi ambazo mnasema zinarudi kwa mgongo wa nyuma, ninataka kuwakumbusha kwamba kodi zote zinazotolewa na halmashauri ni lazima zifanyike kwa kushirikiana na Waziri wa Fedha vinginevyo ni kinyume cha sheria.

"Nikuombe Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Nishati na Madini, zileteni hizo halmashauri serikalini tuje tuziangalie upya," aliagiza.

Mwenyekiti wa Shirikisho wa Vyama vya Madini, John Bina, alitaja baadhi ya kero wanazokumbana nazo kuwa ni mitaji ambapo taasisi za fedha hutoa mikopo kwa wawekezaji wa uchimbaji dhahabu na kuacha kuwasaidia wengine.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alisema uwekezaji mkubwa unaoendelea kwenye utafiti wa madini maeneo mbalimbali ni udhibitisho tosha wa dhamira ya serikali ya kuwekeza katika sekta hiyo.




Naibu Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Mary Masanja, akikata utepe kuzindua andiko la mradi pamoja na mkataba wa makubaliano ya ufadhili wa kuwezesha mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki, jijini Dodoma juzi. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Bunge lamulika usalama mizigo ya wateja bandarini

**Na Gwamaka Alipipi**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imeiagiza Mamlaka ya Bandari (TPA) kuhakikisha inasimamia usalama wa mizigo ya wateja inayoshushwa katika Bandari ya Dar es Salaam.

Vilevile, imewataka watumishi wa TPA kutojifungia ndani, bali watoke kwenda kujifunza katika bandari za nchi zinginezo namna wanavyofanya kazi ili waingie katika mfumo wa ushindani.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Seleman Kakoso, alitoa maagizo hayo jana wakati kamati yao ilipozuru kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

"Mtenge kitengo cha masoko ili kwenda katika nchi zinginezo kutafuta wateja. Bandari ya Dar es Salaam imefanyiwa maboresho makubwa, meli kubwa zinaweka nanga, zinapakua mizigo kwa muda mfupi," alisema Kakoso.

Alishauri asilimia 40 ya mapato yanayokusanywa katika Bandari ya Dar es Salaam yaachwe kwa TPA ili yatumike katika shughuli za maendeleo bandarini huko, badala ya utaratibu wa sasa wa makusanyo yote yanapelekwa serikalini.

Naibu Mkurugenzi Mkuu TPA, Karim Mataka, akizungumzia kuhusu kuondoa urasimu katika Bandari ya Dar es Salaam, alisema:

"Kwa sasa hakuna urasimu bandarini kwa sababu tumekuwa tukishirikiana na mamlaka zinginezo kufanya kazi kama vile Shirika la Reli Tanzania (TRC), Mamlaka ya Mapato (TRA), Shirika la Viwango (TBS) na Wakala wa Barabara (TANROADS).

Alisema kwa sasa wameondoa vizuizi vilivyokuwapo, akitolea mfano kwamba TANROADS wameondoa kero katika mizani iliyokuwa ikilalamikiwa na wafanyabiashara kwa kubakiza mizani miwili pekee kwa ajili ya upimaji.

Kuhusu udanganyifu wa bidhaa kwa wateja pindi wanapoingiza mizigo bandarini, Mataka alisema: "Tumedhibiti hali hiyo. Kwa sasa tuna mashine za ukaguzi nane eneo la bandari, pia tuna mbwa wenye uwezo wa kukagua mizigo na tumefanikiwa kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya."

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Atupele Mwakibete, alisema serikali imefanya maboresho makubwa katika Bandari ya Dar es Salaam kwa kuwa ndiyo uti wa mgongo wa ukusanyaji mapato.

Alisema bandari hiyo imekuwa ikipitisha mizigo mingi kwenda nchi za jirani ikiwamo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) asilimia 37, Malawi asilimia saba, Burundi asilimia tano, Rwanda asilimia saba na Uganda asilimia mbili.

"Mikakati ya serikali ni kuhakikisha soko lote la nchi zisizokuwa na bahari linakamatwa na TPA, mizigo yao yote inapitia Tanzania," alitamba.

# ACT 'yanunua' kesi makada wa CHADEMA waliofungwa

**Said Hamdani,** LINDI.

CHAMA cha ACT-Wazalendo mkoani Lindi, kinajipanga kukata rufani kupinga adhabu ya kifungo waliyopewa wanachama wanne wa CHADEMA Kata ya Majengo, Halmashauri ya Mtama, kwa makosa mbalimbali likiwamo la kuharibu mali wakati wa Uchaguzi Mkuu mwaka 2020.

Tamko la kusudio hilo lilisomwa na Mwenyekiti wa ACT wa Mkoa huo, Rashidi Mchinjita, alipokuwa anatoa taarifa fupi ya hali ya kisiasa mkoani Lindi katika mkutano wa kumtambulisha kwa viongozi na wanachama wa ACT Mwenyekiti wa Taifa, Duni Juma Haji.

Wafuasi hao waliofungwa miaka nane kila mmoja ni Diwani aliyeshindwa uchaguzi mwaka 2020, Rajabu Hassani Mfaume, kampeni meneja wake, Dadi Hassani Shayo, Hamisi Abdallah Malege na Moshi Hamisi Mbelenye.

Mchinjita akiwasilisha taarifa kwenye mkutano huo uliojumuisha viongozi na wanachama kutoka wilaya nne kati ya tano za Mkoa wa Lindi, alisema kufuatia hukumu waliyopewa wafuasi wa Chadema, wanajiandaa kukata rufani.

"Tutakwenda gerezani ili kuzungumza nao ili kushauriana na kufahamu mawakili waliokuwa wanawatetea tuweze kukata rufani," alisema Mchinjita.

Alisema pia watapenda kufahamu mawakili hao maeneo yepi walikwama kuwanusuru wateja wao.

Mwenyekiti huyo alisema pamoja na changamoto zilizopo, zikiwamo za kiuchumi, lakini kufuatia udugu wao na wana CHADEMA wa kuzaliwa na wa kisiasa, wanalazimika kuingilia kati kukata rufani kwa ajili ya kuwanusuru na adhabu waliyopewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi wa Mkoa wa Lindi wiki iliyopita.

Februari 18 mwaka huu, Mahakama hiyo iliwahukumu makada hao wa CHADEMA kutumikia kifungo cha miaka minane kila mmoja, baada ya kupatikana na hatia ya makosa mbalimbali, likiwamo kuharibu mali za umma na binafsi.

Mali zilizoharibiwa kwa kuchomwa moto ni Ofisi ya Serikali Kata ya Majengo na pikipiki moja iliyokuwa inamilikiwa na mtu binafsi na kujeruhi watu watatu akiwamo Askari Polisi WP 7657 Esther Kalaminyo.


**UBALOZI WA SWEDENI, UINGEREZA NA WATAALAM MBALI MBALI**

**MNADA WA HADHARA:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Swedeni, Uingereza na Wataalam mbali mbali watauza kwa mnada wa hadhara Funicha za nyumbani, Magari na Genereta tarehe 26 February, 2022 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

Fenicha na Computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi:Sofa set, Chest drawer,Bamboo sofa,Dining table, Dining chairs , Book case, Meza za ofisi, Viti, Vitanda, Magodoro,Makabati, Fridge, Up Right Freezer, Washer, Dryer, Majiko ya umeme/Gas, Computer set,Porker vibrator, Simtank na vingine vingi.

**Magari na Generator yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Land Cruiser GXL-V8 S.Wagon | D4D Diesel Engine | 2014 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser GXR-V8 S.Wagon | D4D Diesel Engine | 2008 | Umelipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser GX Station Wagon | 1HZ Diesel Engine | 2005 | Haujalipwa |
| 1 | Nissan Patrol Station Wagon | TD42 Diesel Engine | 2008 | Umelipwa |
| 1 | Land Rover Defender S. Wagon (Puma) | SALLDHM Diesel Eng. | 2011 | Umelipwa |
| 1 | Ford Ranger Pick Up Single Cabin | PF2H Diesel Engine | 2016 | Umelipwa |
| 1 | Mercedes Benz Station Wagon | E230 Petrol Engine | 2010 | Umelipwa |
| 1 | Toyota L.Cruiser Prado Station Wagon | 3RZF Petrol Engine | 1998 | Umelipwa |
| 1 | Toyota Verossa Saloon | GX110 Petrol Engine | 2001 | Umelipwa |
| 1 | Isuzu NKR Truck 2 Tons | 4HG Diesel Engine | 1998 | Umelipwa |
| 3 | Generator KVA 6 & 2.7 | Diesel Engine | - | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 23 mpaka 25 February, 2022, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 3 March, 2022 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini na kuwa na barakoa.

**Kwa maelezo zaidi waone:**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA DAR ES SALAAM**
**CELL NO: 0754 284 926**
**E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

216717302

# Usimamiaji sera Bonde Mto Nile wahimizwa

**Na Maulid Mmbaga**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ametoa rai kwa taasisi zenye jukumu la ulinzi na usimamizi wa rasilimali za Bonde la mto Nile (Nile Besin Initiative, NBI) kusimamia sera, sheria, na taratibu zilizokubaliwa na nchi wanachama ili kuhakikisha mto huo unaleta maendeleo kwa wote.

Alitoa rai hiyo jana mkoani Dar es Salaam wakati akihutubia katika mkutano wa maadhimisho ya 16 ya NBI, na kwamba taasisi hizo pia ni muhimu zifuatilie hali ya ikolojia ya mto huo na kufanya utafiti ili kubaini, kudhibiti na kuzuia uchafuzi kutoka maeneo yanayozunguka bonde hilo.

Alisema dunia nzima inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaathiri sekta mbalimbali za kiuchumi na maendeleo ya nchi ya Bonde la Mto Nile, huku akisisitiza kwamba kuna haja ya nchi zote za bonde hilo kuwa makini katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi ili kuhakikisha hayaathiri maendeleo ya mto huo.

"Ili Bonde la Mto Nile liendelee kuwa salama ni muhimu nchi zetu zijidhatiti katika kulinda vyanzo vya maji vinavyochangia uhai wa Mto Nile, pamoja na hayo yote naendelea kusisitiza kuwa ushirikiano ndiyo njia bora zaidi katika kusimamia kwa amani rasilimali zetu za maji, alisema na kuongeza.

"Ushirikiano wenye tija na kuaminiana ndiyo msingi wa kuanzisha mifumo ya pamoja ya usimamizi ikiwamo kuwa na mawasiliano rasmi, kubadilishana takwimu, taarifa na mipango ya usimamizi, kuwa na mipango ya pamoja ya maendeleo na utunzaji wa mifumo ya ikolojia na mazingira na kujenga uwezo wa wataalamu wetu ya pamoja katika nyanja mbalimbali za usimamizi wa rasilimali za maji," alisema Dk. Mpango.

Aliongeza kuwa hayo yote ni muhimu kuyazingatia katika kuhakikisha wanazitumia fursa zitokanazo na bonde la mto Nile kwa faida yao wote huku wakiwa na amani, akidai kuwa nchi wanachama wanajukumu la kuhakikisha wanafikia malengo yao ya ushirikiano waliyojiwekea kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia rasilimali za maji ya mto huo. Aidha, alieleza kuwa miaka 20 iliyopita walianza safari ya kuanzisha kamisheni ya bonde la mto Nile kupitia mkataba wa ushirikiano wa bonde hilo akibainisha kuwa ulisainiwa na kuridhiwa na baadhi yao, akidai kwamba hadi sasa hawajafanikiwa kuunda chombo hicho.

Pia kutokana na hilo alitoa rai kwa nchi wanachama kubeba ajenda hiyo kama ajenda kuu katika ushirikiano wao. Alidai kuwa Tanzania inaamini kwamba uwepo wa kamisheni utaimarisha juhudi zao za pamoja katika usimamizi endelevu na wa pamoja na matumizi ya usawa na uendelezaji wa rasilimali za maji za bonde la mto Nile.

"Kupitia kamisheni hiyo fursa nyingi zitafunguka na tutakuwa tunatuma ujumbe kwa ulimwengu na wadau wa mto naili kuwa sasa tuna nia ya dhati ya kutaka kushirikiana zaidi, na kwa muktadha huu ingependeza sana mwaka ujao 2023 wakati tutakapokuwa tukiadhimisha miaka ya siku ya Bonde la Mto Nile tutakuwa na kamisheni ya mto Nile.

"Mimi naamini tukiamua jambo hili linawezekana lakini kipekee sana ninawasihi kila nchi mwanachama wa Nile Besin Initiotive, (NBI) kuweka msukumo wa pekee kwanza kukuza vyanzo vya maji, kupanda miti na kufanya usafi wa kuzuia utupaji hovyo wa taka ngumu na maji taka (hard solid and liguid waste," alisisitiza Dk. Mpango.

Alikumbusha kuwa dhima ya ushirikiano wa nchi wa bonde la mto Nile imejengwa katika falsafa ya mto mmoja watu wamoja na dira moja, aliendelea kusisitiza kwamba umoja wao unatoa dira moja, nafasi kwa nchi wanachama kuimarisha mfumo wa ushirikiano ambao unachochea maendeleo na usimamizi bora wa rasilimali za bonde hilo kwa faida ya wote.

Alisema mafanikio ya nchi wanachama wa mto Nile katika nyanja za kiuchumi na kijamii ni mafanikio ya Afrika zima, hivyo alisisitiza kuwa ni muhimu kwa wote kuendelea kuzingatia mkataba wa ushirikiano wa bonde hilo kwa maslahi mapana ya kikanda na bara kwa ujumla.

Balozi wa Kenya nchini, Dan Kazungu, alitoa wito kwa nchi wanachama kuimarisha ushirikiano katika masuala mbalimbali yanayohusu utunzaji wa rasilimali maji katika mto huo ili kuleta uwiano katika manufaa yanayotokana na bonde hilo.

Mwakilishi kutoka Rwanda, Verdiane Nyiramana, alisema ushirikiano katika miradi na sera itasaidia kuleta maendeleo kwa nchi wanachama na wananchi kwa kunufaika kwa kupata fursa mbalimbali zinazotokana na Bonde la Mto Nile.




Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, wakisaidia kuwaokoa wafanyakazi wa benki ya NMB, tawi la Mkwawa, mjini Iringa jana, wakati wa zoezi la utimamu na utayari wa kukabiliana na majanga maeneo ya kazi, lililofanyika kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na benki hiyo. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## TCRA yatoa sababu bando kwisha haraka

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema kuongezeka kwa mitandao ya simu na kasi ya simu janja nchini ni miongoni mwa mambo yanayochangia 'bando' kwisha haraka.

Mkurugenzi wa Masuala ya Sekta wa TCRA, Dk. Emmanuel Manasseh, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, wakati wa mkutano wake na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).

Alitaja mambo mengine yanayosababisha kumaliza 'bando' kwa haraka kuwa ni kuongezeka kwa kasi ya mtandao kwenye simu janja mfano kutoka 3G hadi 4G.

Mambo mengine, kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo ni ubora wa video na picha unavyoongezeka unasababisha matumizi nayo kuongezeka.

"Tuna "application" mbalimbali kwenye whatssap zinafanyiwa 'update' mara kwa mara nazo zinatumia data. Watumiaji wengi wa simu kuna vitu vinaendelea kwenye simu yake lakini mtumiaji hajui. Uwapo wa 'application' nyingi, zingine hazitumii hivyo zinamaliza 'bando'," alisema.

Alisema mamlaka hiyo imekuwa ikifanya majaribio mbalimbali ili kuhakikisha watoa huduma wanatoa huduma sawa na walichowaahidi watumiaji.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisema asilimia 27 ya watumiaji wa simu janja nchini ndio wanaonekana kutumia muda mdogo kusoma habari ndefu, hivyo wengi wanaotumia simu hizo hupoteza data bila kujua.

Alisema Tanzania inaongoza kwa kuwa na 'bundle' rahisi na salama Afrika na duniani, hivyo kila mtoa huhuma ana uwezo wa kubadilisha vifurushi kila baada ya siku 90.

"Utafiti mbalimbali duniani unaonyesha kuwa gharama za kupiga simu kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine nchini Tanzania, ziko chini tofauti na nchi nyingine duniani, gharama za kawaida bila kujiunga na kifurushi, pamoja na gharama zilizounganishwa na kifurushi nazo zimeshuka, " alisema.

Dk. Jabiri alisema kabla vifurushi havijabadilishwa, mtoa huduma hupeleka mapendekezo yake TCRA kwa ajili ya kuangalia kama vinaendana na utafiti uliofanyika ili kutomuumiza mlaji au mtumiaji wa huduma za mawasiliano nchini.

# Serikali yaomba msaada vifaa tiba Global Fund

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameuomba Mfuko wa Dunia (Global Fund) kuisaidia Tanzania vifaa tiba ili kwenda sambamba na juhudi za serikali za kujenga miundombinu ya afya kwa kasi ili kuboresha masuala ya tiba kwa wananchi.

Dk. Nchemba alitoa rai hiyo jana Dar es Salaam alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkuu wa Idara ya Afrika wa Global Fund, Linden Morrison, aliyeko nchini kwa ziara ya kikazi. Wawili hao walijadili masuala kadhaa muhimu ya ushirikiano kati ya Tanzania na mfuko huo. "Serikali imewekeza rasilimali kubwa katika ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali ambazo zimejengwa kwa kasi kila mahali nchini lakini changamoto kubwa iliyopo na ambayo tungeomba mtusaidie ni vifaa tiba vya kisasa vitakavyoiwezesha serikali kutoa huduma zilizokusudiwa kwa wananchi," alisema Dk. Nchemba.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan, ameielekeza Wizara ya Fedha na Mipango kutafuta rasilimali fedha itakayotumika kwa ajili kununua vitendea kazi vitakavyokuwa na hadhi ya majengo ya kisasa yanayojengwa hivi sasa na kuwafanya wananchi wapate huduma bora za afya karibu na maeneo yao.

Pia aliushukuru mfuko huo kwa kutoa msaada wa dola za Marekani milioni 721 zitakazotumika kukabiliana na athari za ugonjwa wa UVIKO - 19 katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia Januari, mwaka jana.

Aliishukuru pia Global Fund kwa kutaka kuifanya Tanzania kuwa kituo cha utalii wa kimatibabu ambapo watu mbalimbali kutoka kila pembe ya dunia watakuja nchini kupata matibabu na kuwa sehemu ya utalii huo wa tiba baada ya kuimarika kwa mifumo ya utoaji wa huduma ya matibabu itakayokwenda sambamba na uwepo wa vifaa tiba vya kisasa.

Kwa upande wake, Morrison alipongeza Tanzania kwa kushirikiana na mfuko wake katika kupiga vita maradhi ya Kifua Kikuu, Malaria na Ukimwi pamoja na namna ilivyokabiliana na ugonjwa wa UVIKO - 19 kwa umahiri mkubwa.

Aliahidi kuwa Mfuko wa Dunia utaendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kukabiliana na magonjwa hayo kwa kuelekeza rasilimali fedha kwa ajili ya kununua dawa pamoja na kuboresha mifumo ya utoaji huduma ya afya ikiwamo kuboresha mifumo ya utoaji huduma ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA).

Tangu Global Fund ianze kushirikiana na Tanzania kukabiliana na maradhi ya Kifua Kikuu, Malaria na Ukimwi mwaka 2002 hadi sasa, mfuko huo umetoa msaada wa dola za Marekani bilioni 1.9.

Katika ziara yake, Morrison aliambatana na Nelson Msuya, Mwakilishi wa Global Fund-Tanzania na kwa upande wa Tanzania alikuwapo Kamishna wa Madeni wa Wizara ya Fedha na Mipango, Japhet Justine, Kamishna wa Fedha za Nje, Sauda Msemo na Ofisa wa Dawati wa Global Fund wa Wizara hiyo, Mukajungu Kamuzora.

TANGAZO




# Jinsi nilivyoshinda KIKUBWA kwa mara ya pili betPawa

**Mimi ni Martin, mjasiriamali, mkulima na mshindi MKUBWA wa betPawa mara 2. Nilibashiria TSh500 kwenye mechi 8 sare na nikashinda TSh5,834,741. Hiyo iliongezwa hadi TSh7,293,926.25 (kabla ya kodi) kwa bonasi ya ushindi 25% ya betPawa. Hii ni hadithi yangu...**

Nilifanya utafiti wa kina kabla ya kuweka bashiri. Kabla ya michezo kukamilika, nilisinzia. Nilipoamka na kuingia kwenye akaunti yangu, ilikuwa na ushindi wangu tayari. Nilifurahi sana siwezi kuelezea.

Nataka kununua ardhi ili kupanua shughuli zangu za kilimo, pia nitaongeza mtaji kwenye shughuli zangu za ujasiriamali ili kufanya mambo kuwa MAKUBWA zaidi.

Hii ni mara ya pili nimeshinda KIKUBWA. Mimi nina ushuhuda kwamba betPawa ni waaminifu na utapata pesa yoyote utakayoshinda bila matatizo yoyote.

**Pata nafasi kushinda KIKUBWA leo kwenye betpawa.co.tz**

betPawa

*Cheza kiasi. 18+. betPawa imesajiliwa chini ya bodi ya michezo ya kubashiri ya Tanzania. Leseni #SBI000000026*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Lakufungia mwandishi liangaliwe kwa makini

**JUZI** Waziri wa Habari, Mawasiliano na Tekonolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema moja ya maboresho ya Sheria ya Huduma za Habari, 2016, ni kutofungia chombo cha habari bali mwandishi aliyeandika habari yenye utata.

Alisema kinapofungiwa chombo cha habari ni hasara kwa nchi, pia inaathiri wengi ambao hawahusiki kama wafanya usafi na wauzaji wa magazeti na ndiyo maana wanaona sasa ni muhimu kushughulika na mwandishi.

Tunampongeza waziri kwa kuona hilo kwa kuwa kufungia vyombo vya habari kumesababisha hasara hata kwa serikali yenyewe ambayo ingekusanya mapato kutoka kwa kampuni za wafanyakazi walioajiriwa, lakini pia wategemezi au maskini waliongezeka.

Kilio cha wadau wa habari na taasisi zake kimekuwa kikubwa muda mwingi, na wengi wamepinga uamuzi wa kufungia chombo kizima cha habari, lakini sasa linakuja jambo jingine la kumwadhibu mwandishi aliyeandika kilichosababisha matatizo.

Taasisi za wanahabari zimepaza sauti ikiwamo kuchambua sheria hiyo na nyingine zinazosimamia tasnia ya habari nchini, kwa kuainisha faida na hasara za baadhi ya vifungu, kwa namna gani vinaminya uhuru wa vyombo vya habari na kutoa mapendekezo ya nini kifanyike.

Tunatambua kuwa Nape alikuwa waziri kwenye wizara hiyo hiyo wakati sheria hiyo inatungwa, alikaa kando kwa muda tunaamini alipata nafasi ya kutathmini, kujitathimini na kuona namna sheria inavyofanya kazi. Lakini tunaamini alisikia kilio cha wadau wengi kuhusu sheria hiyo, na tunaamini hata sasa atatoa nafasi kwa wadau wote wa habari (taasisi za habari zaidi ya 12 na wanahabari wenyewe) kuzungumza naye, kuhusu mambo mbalimbali ambayo kimsingi yanakwaza utendaji kazi wao.

Tunakubalinana kuwa kufungia chombo cha habari ni kuumiza wengi, lakini lazima sasa tunapofikia uamuzi wa kumfungia mwandishi tuufahamu utendaji kazi wa vyombo vya habari.

Kwa mujibu wa utendaji wa vyombo vya habari kwenye gazeti, mwandishi hana mamlaka ya kuamua kichwa maudhui ya habari yake wala kichwa cha habari zaidi atapendekeza tu, lakini siyo lazima kitumike hicho.

Aidha, mwandishi wa habari hana mamlaka ya habari yake itoke ukurasa gani, kwa uzito gani na eneo gani, hawezi kuamua ipi ikae mbele au wapi, yote jukumu la wahariri.

Wajibu wa mwandishi wa habari unaanzia kwenye kupewa kazi ya kufanya au kuwa na wazo la kutekeleza ambalo atajadiliana na mhariri, ndipo ataendelea kukusanya taarifa na zitakapokamilika atatakiwa kurudi tena kwa mhariri aliyempa kazi kwa mrejesho ndipo watakubaliana cha kuandika.

Habari inapotoka mikononi mwa mwandishi ni mali ya chombo cha habari na ndiyo maana walioajiriwa hawaruhusiwi kupeleka kwenye chombo zaidi ya kile alichoingia nacho mkataba, lakini kwa ambaye hajaajiriwa baadhi ya vyombo hawataki wasambaze kwingine kwa kuwa kuna mashindano ya kibiashara.

Mwandishi anapokabidhi habari kwenye chombo cha habari kupitia mhariri ambaye kitaalam anatambulika kama (gate keeper) kazi yake ni kuisoma kuangalia matakwa ya sheria, kanuni, sera ya chombo cha habari na weledi wa taaluma kabla ya kuruhusu itoke kwenye chombo cha habari.

Ndani ya chombo cha habari kuna kikao cha uhariri ambacho hukutana asubuhi kwa ajili ya kupanga mipango ya siku hiyo kwamba gazeti litoke na habari gani, kisha kikao cha jioni hujadili zote zilizopatikana na kuamua kitu gani kiongezwe au kipunguzwe ili kuhakikisha inakidhi vigezo muhimu.

Kwa mtiririko huo haitoshi kumwadhibu mwandishi mwenyewe kwa kuwa mhariri wake anabeba dhamana anapaswa kujiridhisha na maudhui yote anayoletewa kama yanakidhi matakwa ya kisheria, kitaaluma na sera ya chombo husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanaohujumu mikopo ya halmashauri wanangoja nini?

Na Sabato Kasika

**HALMASHAURI** zinatenga asilimia10 ya mapato ya ndani, kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na wanaoishi na ulemavu.

Katika mgawanyo huo wanawake na vijana hupata asilimia nne wakati asilimia mbili ni kwa wanaoishi na ulemavu ili kufanyia shughuli mbalimbali za ujasiriamali na biashara mijini na vijijini.

Kabla ya kutolewa mikopo, halmashauri hutoa tangazo kwa umma na kuvitaarifu vikundi vya walengwa ambavyo vimesajiliwa kuhusu kuwapo fedha zilizotengwa kwa ajili yao.

Hata hivyo, kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa baadhi ya walengwa wakidai kuzungushwa wanapohitaji mikopo hiyo na wengine kuwatuhumu baadhi ya watumishi wa halmashauri kuwa na 'vikundi hewa'.

Aidha, hudaiwa kuwa baadhi ya watumishi hao hutumia vikundi hivyo kujikopesha fedha hizo huku walengwa wakikosa na kusababisha waone kuwa wanatengwa kwenye mikopo hiyo.

Kilio cha ubadhirifu wa fedha za mikopo inayotolewa na halmashauri kwa vikundi hivyo, hivi karibuni kilifika bungeni, ambapo sasa wadau wanashauri sekta binafsi zihusishwe katika kamati za mikopo na utoaji elimu ya biashara ili kuondokana na tatizo hilo.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), David Silinde, anakiri kuwapo ubadhirifu katika mikopo hiyo, na kufafanua kuwa wanakusudia kubadili sheria na kanuni za mikopo hiyo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri.

Anasema, serikali italeta marekebisho ya sheria na kanuni za jinsi ya utoaji wa fedha hizo kwenye halmashauri na kwamba imesikia kilio cha wabunge na kuwa, inawezekana mfumo wa sasa si rafiki.

Kwa kauli hiyo ya Naibu Waziri, ni vyema hatua hiyo ya marekebisho ikaharakishwa ili walengwa wanaondokane na kilio hicho cha muda mrefu cha kukosa mikopo bila sababu za msingi.

Wabunge wamejadili kwa kina wakilalamikia ubadhirifu wa fedha hizo na kuitaka serikali isitishe mikopo hiyo, kwa kuwa imetengeneza mianya ya rushwa na ufisadi kwenye halmashauri.

Hivyo ni kweli kwa mazingira hayo na jinsi hata baadhi ya walengwa wamekuwa wakilalamika, kuna haja ya kuchukua hatua ambazo zitasaidia kumaliza tuhuma hizo ili walengwa wanufaike.

Inaelezwa kuwa katika utaratibu huo wa kukopeshana huku walengwa wakiachwa pembeni, umekuwa ukisababisha kutorejeshwa kwa mikopo na hivyo kukwamisha juhudi za serikali za kukwamua makundi hayo kiuchumi.

Kila mara wito umekuwa ukitolewa wa kuwataka walengwa kuchangamkia mikopo hiyo, lakini wanapokutana na vikwazo vya aina hiyo, ni wazi kwamba wanaweza kukwama na hatimaye kukata tamaa.

Ninaamini, walengwa wakipewa mikopo, kuna uwezekano wakairejesha kwa wakati na hivyo kusaidia mzunguko wa fedha hizo kuwafikia wengine ambao watakuwa kwenye foleni ya kusubiri kukopeshwa.

Lakini pia kelele za wabunge kuhusu ubadhirifu wa fedha hizo zingewashtua wale ambao wamekuwa wakijihusisha na mchezo huo na kuuacha ili taratibu zichukue nafasi yake badala ya kutumia njia ya mkato.

Kwa ujumla fedha hizo zinatakiwa kuwa mkombozi wa kuinua pato la maisha kwa wananchi kama ilivyokusudiwa, lakini kwa ujanja unaodaiwa kufanywa na watumishi wachache, lengo haliwezi kufikiwa.

Bila kuwapo kwa hatua madhubuti za kukabiliana na kile ambacho kimekuwa kikilalamikiwa, ni wazi kwamba fedha hizo hazitaweza kubadilisha maisha ya walengwa ambao ni wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Inaumiza kusikia madai kwamba fedha hizo zinaishia mikononi mwa watendaji na watumishi wachache badala kuwakopesha walengwa ili waweze kujikomboa kimaisha kupitia mikopo ya halmashauri zao.

Hivyo ni vyema mikopo hiyo ya halmashauri ikawanufaisha walengwa, ili kuondoa malalamiko na tuhuma za muda mrefu ambazo zinawagusa baadhi ya watendaji na watumishi kwamba wanajinufaisha wao.

## WCF yawezesha wasioona machapisho

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeikabidhi Jumuiya ya Maendeleo kwa Wasioona Tanzania (TAB) machapisho ya nukta nundu pamoja na fimbo nyeupe katika kuunga mkono maendeleo ya watu wenye mahitaji maalumu.

Makabidhiano hayo yalifanyika jijini Dodoma wakati wa maadhimisho ya Siku ya maandishi ya nukta nundu ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda.

Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, alisema katika kutekeleza majukumu yake, WCF imeendelea kushirikiana na makundi maalumu wakiwamo watu wasioona kwenye masuala mtambuka ikiwemo elimu.

"Tunatambua kuwa kundi hili linakabiliana na changamoto ya kupata taarifa kwani machapisho mengi hutolewa katika maandishi ya kawaida, WCF imechapisha miongozo inayotoa elimu ya fidia kwa wafanyakazi kwa nukta nundu (braille) kwa ajili ya wale ambao hawawezi kusoma maandishi ya kawaida." alifafanua.

Alisema mfuko unatambua wanachama wasioona ni miongoni mwa wadau muhimu sana chini ya Wizara ya Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu ambao wapo katika kada mbalimbali nchini kote na miongoni mwao ni waajiriwa wa sekta ya umma na sekta binafsi.

Zaidi ya machapisho hayo, WCF imekabidhi pia fimbo nyeupe ili kuwarahisishia kundi hilo utekelezaji wa majukumu ya kila siku katika kujenga uchumi wa Taifa letu.

Prof. Mkenda aliipongeza WCF kwa kushirikiana na kundi hili maalum kwani hatua hiyo inaendana na nia ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuzitaka Taasisi za Umma kuboresha huduma na kuleta maendeleo kwa wananchi.

Alisema kuwa Serikali ipo katika hatua za mwisho za uchapaji vitabu vya maandishi ya nukta nundu kwa shule za sekondari pamoja na wanafunzi wasioona kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne kwa masomo ya sanaa, sayansi, biashara na elimu ya awali.

# Machinga milioni 2 bado kupewa vitambulisho

Na Augusta Njoji, DODOMA

SERIKALI imesema hadi sasa vitambulisho vya wajasiriamali wadogo (machinga) milioni 1.6 vimetolewa huku milioni 2.1 bado wakiwa hawajapatiwa vitambulisho hivyo.

Aidha, imewaonya kuacha kutumika kwa maslahi ya watu binafsi na badala yake wajikite kwenye shughuli za kujikwamua kiuchumi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Zainabu Chaula, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua kikao kati ya wizara na viongozi wa Shirikisho la Umoja wa Machinga nchini kilichofanyika jijini hapa.

Alisema kwa sasa serikali inaendelea na mikakati ya kuwapatia vitambulisho vyao wajasiriamali milioni 2.1 waliobaki.

"Taarifa zilizopo mpaka sasa vitambulisho vilivyotolewa ni milioni 1.6 kati ya machinga milioni 3.7 waliopo. Sasa tunataka hawa waliobaki milioni 2.1 tunawapataje kuwapa vitambulisho ndiyo maana tunatembea na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili watuambie mchakato ulikuwaje tuukimbize maana hili ni kundi kubwa,"alisema.

Dk. Chaula alibainisha kuwa mifumo ya serikali ni endelevu, hivyo pamoja na kuhamishiwa kwenye wizara hiyo kutoka TAMISEMI, wataendelea kutambuliwa.

"Suala la kutambuliwa si kwamba walikuwa hawatambuliwi. Walitambuliwa na walipata usaidizi wote unaostahili isipokuwa kwa sababu imeanzishwa wizara mpya yenye mambo mahususi," alisema.

Kuhusu kutumiwa, Dk. Chaula alisema: "Kundi hili ni kubwa, hivyo wasitumiwe kwa aina yoyote badala yake wafanye kazi ya kujikwamua kiuchumi. Hatutakuwa na mgogoro wowote na machinga zaidi ya kufanya kazi kwa pamoja katika ustawi wa nchi yetu."

Akizungumzia Sh. bilioni tano zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kundi hilo, Katibu Mkuu huyo alisema zimeelekezwa kwenye kuboresha miundombinu yao na kwamba TAMISEMI wanaendelea kulishughulikia hilo.

"Ule mgawanyo ulishatolewa kwa ajili ya kuonyesha miundombinu na mchakato unaendelea. Nina imani tukimaliza haya tutajua tunatokaje TAMISEMI wataendelea na uratibu," alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Amon Mpanju, alisema kikao hicho cha siku mbili ni cha kupokea kundi hilo kutoka TAMISEMI na watapitishwa kwenye masuala ya uongozi, namna wanavyojiongoza, mifumo na mbinu mbalimbali za mawasiliano,pamoja na sheria,taratibu na kanuni za kuongoza umoja wao.

Naye Mwenyekiti wa Shirikisho hilo, Ernest Matondo, alisema wanakabiliwa na kero ya miundombinu kwenye masoko na hivyo kuomba mchakato wa matumizi ya Sh. bilioni tano zilizotolewa na Rais Samia uharakishwe ili wafanye biashara kwenye mazingira mazuri.

"Miundombinu kwenye masoko haijakaa vizuri kwa kuwa kuna fedha tumeambiwa zimetengwa kwa ajili ya miundombinu ya machinga. Tunaomba sasa ziruhusiwe ziende kwenye miundombinu ili machinga wafanye kazi katika mazingira mazuri," alisema.

"Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kulitambua kundi hili maalum na kutupatia wizara. Hili ni jambo la kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Nishukuru benki ya NMB kwa kutenga Sh. bilioni 200 kwa ajili ya wajasiriamali kukopeshwa ndani ya miaka mitano na tayari tumeshatia saini makubaliano,"alisema.



Meneja wa Shirika la ugavi la umeme nchini (TANESCO), mkoa wa Arusha, Herini Muhina, akizungumza na wananchi wa Kata ya Terati, Wilayani Arusha, kuhusu zoezi la kuwaunganishia umeme wateja 73 waliofanya malipo yao linalitarajiwa kukamilika ndani ya wiki hii. PICHA: WOINDE SHIZZA

# Ushirika wajitosa hamasa chanjo UVIKO-19

Na Sabato Kasika

VIONGOZI wa Bodi ya Chama cha M

singi cha Ushirika umoja cha mjini Liwale, mkoani Lindi, kimejitosa kwenye kampeni ya kuhamasisha wanachama wa chama hicho kupata chanjo ya UVUKIO-19.

Mwenyekiti wa chama hicho, Hassan Myao alisema walianza kampeni hizo Desemba mwaka jana mara baada ya wao kupata chanjo hiyo na sasa wanaelekeza nguvu kwa wanachama wao. "Tunaendesha kampeni hiyo na wale ambao wanakuwa tayari kuchanjwa, wanatuambia, nasi tunafikisha ujumbe kwa watu wa chanjo wanawafuata huko vijijini ili kuwachanja," alisema Myao.

Alisema, kampeni yao imesaidia kubadilisha mawazo ya baadhi ya wanachama ambao awali walikuwa wakiiona chanjo kama kitu cha hatari, ambapo sasa wameanza kujitokeza kuchanja.

"Hata mimi nilikuwa sitaki kabisa kusikia chanjo ya corona, lakini baada ya kuelimishwa nikaelewa, nikawaelimisha wajumbe wote nane wa bodi tukachanjwa, na sasa tunaelekeza nguvu kwa wanachama,"alisema.

Alisema chama hicho kina wanachama 1042 ambao wengi wao wanaishi vijiji mbalimbali vya wilaya ya Liwale, na kwamba mwanachama ambaye anayekuwa tayari kuchanjwa anapiga simu ili watu wa afya waende kumchanja.

"Mwanachama anapiga simu kwetu nasi tunafikisha taarifa kwa watu wa afya na kuwalekeza aliko na wakati mwingine watu wanachanjwa wakiwa shambani au nyumbani kutegemea watakutwa katika mazingira gani," alisema.

Alisema, ingawa si jukumu lao kujua idadi ya watu waliochanjwa, lakini anaamini kuwa katika mkutano mkuu wa mwaka wa chama hicho unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao, watakuwa na la kusema kuhusu chanjo. Mwenyekiti huyo alisema, chanjo ni hiari, na kwamba inawezekana wakawapo wale wanaotaka kuchanja, lakini wakawa hawajapata taarifa sahihi kuhusu umuhimu wa kuchanja.

"Hivyo, busara inanielekeza kwamba kuna kuwa na haja ya kuulizana jambo hilo, na ikiwezekana, basi chanjo ziletwe kwenye mkutano huo, ili mwanachama atakayekuwa tayari achanjwe," alisema.

# Kesi ya vigogo UDART miaka mitatu upelelezi bado kabisa

Na Kulwa Mzee

UPELELEZI wa kesi inayomkabili aliyekuwa Mkurugenzi wa Miradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (UDART), Robert Kisena na wenzake, bado haujakamilika licha ya kwamba imepita miaka mitatu tangu ilipoanza.

Kutokana na hali hiyo, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu , imeutaka upande wa Jamhuri kuharakisha upelelezi kwa kuwa ni muda mrefu sasa.

Hakimu Mkazi Mkuu Ritha Tarimo alitoa amri hiyo jana wakati kesi hiyo ilipotajwa mbele yake na washtakiwa wote walikuwapo.

Upande wa Jamhuri walidai upelelezi unaendelea wakiwa katika hatua za mwisho na waliomba tarehe nyingine ya kesi kutajwa.

"Harakisheni upelelezi ukamilike. Ikifika Mei kesi itakuwa na miaka mitatu upelelezi haujakamilika," alisema Hakimu Tarimo na kuahirisha kesi hadi Machi 23, mwaka huu.

Washtakiwa katika kesi hiyo, mbali na Kisena ni mkewe Florencia Mashauri, Kulwa Kisena, Charles Newe na Chen Shi.

Kisena na wenzake waliondolewa mashtaka ya kutakatisha fedha Septemba 13, 2019 na kubakiwa na mashtaka ya uhujumu uchumi ikiwamo kusababisha hasara ya Sh bilioni 2.4 kwa kampuni hiyo.

Katika hati mpya washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 15 kati ya 19 ikiwamo kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kuisababishia Udart hasara ya Sh 2,414,326,260.70.

Inadaiwa kuwa kati ya Oktoba 2012 mpaka Mei 31, 2018 washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo.

Inadaiwa kati ya Januari Mosi, 2011 na Mei 31,2018 katika maeneo tofauti wakiwa na watu wengine waliratibu shughuli za kiharifu huku wakijua kufanya hivyo ni kosa la kisheria.

Kati ya Januari Mosi ,2015 na Desemba 31,2017 inadaiwa kuwa katika eneo la Jangwani, washtakiwa hao wakiwa na Mkurugenzi wa Kampuni ya Zenon Oil Gas Limited, walijenga kituo cha mafuta kinachoitwa Zenon Oil and Gas katika karakana ya kampuni ya UDART bila kuwa na kibali kutoka Mamlaka ya Uthibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA).

Pia ilidaiwa kati ya Januari Mosi, 2015 na Desemba 31,2017 katika eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam, washtakiwa wakiwa na wakurugenzi wa kampuni hiyo kwa pamoja walianzisha biashara ya kuuza mafuta ya petroli katika eneo ambalo halijaruhusiwa.

Shtaka lingine, inadaiwa kati ya Mei 25,2015 na Desemba 31, 2016 katika jiji la Dar es Salaam washtakiwa Robert Kulwa, Charles na Frolencia wakiwa na lengo la kuficha uhalisia waliiba mafuta yenye thamani ya Sh 1, 216, 145, 374 kwa kuyauza wakati wakijua mafuta hayo ni mali ya UDART.

Inadaiwa kati ya Mei 25, 2015 na Desemba 31, 2016 jijini Dar es Salaam kwa makusudi waliisababishia hasara UDART ya Sh 2.414, 326, 260.70.

Washtakiwa wanadaiwa Juni 8,2016 katika Benki ya NMB tawi la Benki House lililopo Ilala jijini Dar es Salaam Robert na Chen walijipatia Sh Milioni 594.9 mali ya mradi huo.

Katika shtaka la mwisho, washtakiwa wote wanadaiwa kuwa kati ya Mei 25,2015 na Desemba 31,2016 walisababisha hasara ya Sh. bilioni 2.4.



Katibu wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Dk. Adolf Rutayuga (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mabadiliko ya jina la baraza hilo ambalo awali lilikuwa likifahamika kama Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Kulia ni Mkurugenzi wa Habari, Utafiti na Mipango wa Baraza hilo, Dk. Marcelina Bailwake, na Mwanasheria wa Baraza, Rosemary Muze. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# NACTE yaongezewa majukumu elimu ufundi

Na Mary Geofrey

BARAZA la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) limefanyiwa maboresho ya sheria mbalimbali za Bunge Namba 4 ya Mwaka 2021, iliyorekebisha Sheria ya Baraza, Sura 129 na kubadili jina na kuwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET)

Katibu Mtendaji wa NACTE, Dk. Adolf Rutayuga, akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, alisema mabadiliko hayo madogo yameliongezea baraza majukumu.

"Baraza limeongezewa jukumu la urekebu na udhibiti ubora wa mafunzo ya ufundi stadi ambayo awali yalikuwa yakifanyika chini ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)," alisema Dk. Rutayuga.

Alisema lengo la marekebisho hayo ni kuongeza ufanisi katika usimamizi, urekebu na udhibiti ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi yanayotolewa nchini. Kutokana na mabadiliko hayo ya sheria, jukumu la urekebu na udhibiti ubora wa mafunzo ya ufundi stadi yamehamishiwa rasmi kutoka VETA na kupelekwa NACTVET.

Dk. Rutayuga pia alisema kuanzia sasa maombi yote ya usajili wa vyuo au vituo vya mafunzo ya ufundi stadi yawasilishwe NACTVET ambako majukumu haya yamehamishiwa.

"Baraza pia linatoa wito kwa vituo au vyuo vyote vilivyosajiliwa kutoa mafunzo ya ufundi stadi kuendelea kuendesha mafunzo hayo kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni zilizopo.

Baraza litaendelea kushirikiana na wadau wote, ikiwa ni pamoja na vyuo katika kuendeleza na kukuza utoaji wa elimu bora kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu," alisisitiza.

## Askofu awaamsha vijana usingizini

Na Renatha Msungu, DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheli Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Amon Kinyunyu, amewataka vijana wasio na ajira kujiepusha na kuacha kukaa vijiweni kwa kuwa wanadumaza akili, hivyo kushindwa kujikwamua kiuchumi.

Kinyunyu aliyesema hayo jana alipokuwa akifungua Mkutano wa Vijana wa Ushiriki, Ujenzi na Utunzaji wa Amani, kupitia uhusiano wa kiuchumi

na kitamaduni kwa maendeleo endelevu, uliofanyika jijini hapa.

Alisema vijana wanapaswa kuacha fikra za kukaa vijiweni kupoteza muda kuzungumza mambo yasiyofaa ambayo yanachangia kuwadumaza

akili ya kubuni miradi mbalimbali ya msingi ya kufanya, ambavyo itawafanya wajikwamue kiuchumi.

"Nawaomba vijana jengeni tabia ya kujituma na kuacha kukaa vijiweni kujadili masuala yasiyo ya msingi. Fanyeni kazi kwa bidii ili kupunguza

malalamiko yanayochangia uvunjaji wa amani kati yenu," alisema Askofu Kinyunyu.

Pia alisema wajibu walio nao vijana hivi sasa ni kulinda amani iliyopo na kutumia nguvu zao kufanya kazi ambazo zitasaidia kuleta maendeleo kwao na kwa taifa.

Pamoja na hayo, alisema wanapaswa pia kutumia fursa zilizopo na elimu waliyopata darasani kama chachu ya kubuni miradi mbalimbali ya maendeleo.

Naye Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Amani mkoani hapa, Sheikh Kisusu Mwangonga, aliwataka vijana kuwa na sauti moja katika utekelezaji wa maendeleo ili kudumisha amani iliyopo nchini.

Alisema vijana hawana sababu ya kutoa maneno machafu mbele ya jamii kama hawana uhakika nayo,isipokuwa wanatakiwa kuelimishana na kujengea uwezo wenzao ambao hawana uelewa na jambo linalozungumziwa kuhusu amani na maendeleo yaliyopo.

Mmoja wa washiriki wa semina hiyo, Samuel Mahazi, alisema vijana wanapaswa kuamka na kutumia teknolojia kwa ajili ya

kuleta maendeleo katika taifa.

"Naomba vijana wenzangu tutumie mafunzo haya kama chachu ya kwenda kubadilika katika ufanyaji wa maendeleo. Tusitumie teknolojia hiyo

kufanya maovu. Nafasi tuliyopewa vijana na serikali tuitumie vizuri ili kuchagiza maendeleo yanayofanywa na serikali," alisema.

HABARI KITAIFA

# Njaa yaleta matokeo mabaya shuleni

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WALIMU wa shule za msingi na sekondari Pandagichiza wilayani Shinyanga, wamesema tatizo la wanafunzi kutembea umbali kwenda shuleni na kurudi pamoja na kushinda na njaa kunachangia kushindwa mitihani yao ya darasa la saba na kidato cha nne.

Walibainisha hayo juzi kwa nyakati tofauti, wakati wakizungumza na Nipashe na kusema kuwa wanafunzi wa maeneo hayo ya vijijini, huwa wanatoka umbali mrefu kuanzia kilomita 5 hadi 10 pamoja na kushinda njaa shuleni.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi ya Pandagichiza wilayani Shinyanga, Laurent Richard, alisema kwenye matokeo ya mtihani wa darasa la saba mwaka jana hawakufanya vizuri kutokana na wanafunzi kushinda na njaa.

Alisema kipindi cha nyuma wanafunzi walipokuwa wakila chakula shuleni walikuwa wakifanya vizuri kitaaluma, lakini kwa sasa baada ya kukosa huduma hiyo wamekuwa hawaelewi masomo yao.

"Matokeo ya mtihani wa taifa wa darasa la saba uliofanyika mwaka jana kulikuwa na wanafunzi 50, na kati ya hao waliofaulu ni 23 na waliofeli 27, matokeo ambayo ni mabaya na hii inatokana na wanafunzi kutokula chakula shuleni na wengine kutoroka vipindi kwenda kula nyumbani kwao na wakienda hawarudi kutokana na umbali," alisema Richard.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Pandagichiza wilayani Shinyanga, George Vangilisasi, alisema shule hiyo inalima mazao mbalimbali kwa ajili ya chakula cha wanafunzi.

Alisema ili watoto waweze kusoma na kuelewa masomo yao vizuri, lazima wapate chakula kwa sababu wengine wanatoka umbali mrefu, hivyo wanapokuwa na njaa hawawezi kuelewa kitu darasani hususani vipindi vya mchana.

Alisema mwaka jana katika shule hiyo, wanafunzi waliopata daraja la kwanza walikuwa 2, la pili walikuwa 6, la tatu 18 na la nne 68 huku waliopata ziro ni 34.

Ofisa Elimu Sekondari wa Pandagichiza wilayani Shinyanga, Irene Edward, alisema kutokana na wanafunzi kufanya vibaya kwenye mitihani yao mwaka jana, mkakati uliopo kwa sasa ni kutoa kipaumbele kwa kutoa chakula.

# TANESCO sasa kuvuna bil. 5/- GGML kila mwezi

**Na Mwandishi Wetu**

KUKAMILIKA kwa mradi wa kupeleka umeme kwenye Kampuni ya uchimbaji madini ya dhahabu ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kunatarajiwa kutaliwezesha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kupata shilingi bilioni tano kwa mwezi zitakazotokana na mauzo ya umeme.

Hayo yamebainika juzi Februari 21, 2022 wakati wa shughuli ya utiaji saini mkataba wa mauziano ya nishati ya umeme kati ya TANESCO na GGML.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika mjini Geita, Mkurugenzi Mtendaji TANESCO, Maharage Chande, alisema kuanza kwa biashara hiyo kutaiwezesha TANESCO kuongeza mapato yatakayosaidia kuboresha huduma mbalimbali kwa wateja wao.

"Maana ya pili tutapunguza uzalishaji wa hewa chafu ya dizeli, lakini pia kuongeza ufanisi wa kazi zao GGML kwa maana ya gharama za uzalishaji zitapungua," alisema Chande.

Aliongeza kuwa, hatua hiyo kubwa na muhimu ya GGML kuunganishwa na umeme wa gridi ya Taifa imefikiwa baada ya miaka zaidi ya ishirini tangu kuanzishwa kwa kampuni ya GGML.

Kufanikiwa kwa jambo hilo kumetokana na jitihada mbalimbali zilizofanywa na TANESCO katika kuimarisha upatikanaji wa umeme ndani ya Mkoa wa Geita kwa kujenga kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Mpomvu chenye uwezo wa megawati 90.

Kwa upande wake Makamu wa Rais wa GGML, Simon Shayo, alisema GGML watajenga kituo cha kupokea na kupoza umeme ambazo zitatumika kwa matumizi ya mgodi.

"Kwetu sisi tunapunguza gharama za uzalishaji wa umeme tunao utumia kwa maana kwa kuacha kutumia mafuta lakini pia kutunza mazingira, Dunia sasa inatoka kwenye matumizi ya mafuta ambayo yanazalisha hewa ya ukaa," alisema Shayo.

Kampuni ya GGML kwa sasa inatumia Dola za Marekani senti 19 kuzalisha umeme kwa unit moja kwa kutumia mafuta, lakini mradi huo ukikamilika na kuunganishwa na gridi watatumia senti 9 za kimarekani kwa unit moja kupata umeme.

Mradi huo wa kupeleka umeme GGML unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu, ambapo utajumuisha njia ya kusafirisha umeme umbali wa kilometa 6 na kituo cha kupoza umeme cha GGML cha kilovolt 33.



Mkurugenzi Mtendaji TANESCO, Maharage Chande, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mradi wa kupeleka umeme kwenye Kampuni ya Geita Gold Mining (GGML) ambao utaiwezesha TANESCO kupata shilingi bilioni tano kwa mwezi. Katikati ni Makamu wa Rais wa GGML, Simon Shayo.

# Tarimba ahimiza vita ukatili kingono

**Na Sabato Kasika**

Mbunge wa Kinondoni Dar es Salaam, Abbas Tarimba, ameitaka jamii kutojitenga na vita dhidi ya unyanyasaji na udhalilishaji wa kingono badala yake iungane na wadau wanaoendesha kampeni za kutokomeza vitendo hivyo.

Tarimba alisema hayo juzi wakati akifungua warsha ya kutoa mrejesho wa awali kuhusu utekelezaji wa mradi wa majaribio ya kukabilina na ukatili wa kingono unaofanyika katika kata za Makumbusho na Mwananyamala wilayani humo.

Mradi huo unatekelezwa na Kituo cha Haki za Binadamu (LHRC), kwa kushirikiana na Shirika la Maendele la Japan (JICA), ambapo jana ulifanyika mrejesho huo ulioshirikisha wadau mbalimbali.

Akifungua warsha hiyo, mbunge huyo alisema vitendo hivyo vimekithiri na kwamba baadhi ya watu wanadhani vinapaswa kudhibitiwa na kundi fulani, hali ambayo inachangia kufanya viendelee kuwapo.

"Wito wangu ni kwamba jamii isijitenge na vita dhidi ya vitendo hivi, kila mmoja kwa nafasi yake ashiriki kwa kukemea na hata kutoa taarifa kwa vyombo vya dola ili hatua zichukuliwe," alisema Tarimba.

Mbunge huyo pia aliwaomba viongozi wa dini kupenyeza ujumbe unaosaidia kuepuka vitendo hivyo, wanapokuwa katika nyumba za ibada, ili kusaidia jamii kubadili tabia.

Awali akimkaribisha mgeni huyo, mratibu wa mradi, Dk. Geofrey Chambua, alisema, umesaidia kuwajengea uwezo watumishi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mwananyamala wakiwamo madaktari, wauguzi, wataalamu wa maabara na watumishi wa kada nyingine zinazoendana na mradi.

"Mradi pia umewajengea uwezo askari polisi zaidi ya 50, wa Dawati la Jinsia na Watoto katika Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni, wa jinsi ya kushughulikia kesi za udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono," alisema Dk. Chambua.

Pia alisema, mradi umetoa mafunzo kwa watendaji na wenyeviti wa serikali za kata na mitaa yote 13 ya Mwananyama la Makumbusho, na kwa waajumbe zaidi ya 50 wa Kamati ya Mkakati wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWA) katika kata hizo mbili.

"Matarajio yetu ni kuona mradi unakuwa msaada kwa manusura wa udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono na kutoa elimu kwa jamii katika kata hizo, ili kupambana na kutokomeza vitendo hivyo na kuhakikisha huduma na haki kwa walengwa zinapatikana kwa ufanisi na wakati muafaka," alisema.

Naye Mrakibu Mwandimizi wa Polisi (SSP), kutoka Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Leah Mbunda, alisema Jeshi la Polisi litaendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha vitendo hivyo vinakomeshwa ndani ya jamii.

"Takwimu za LHRC zinaonyesha kuwa Kinondoni inaongoza kwa vitendo hivyo, lakini ninaamini ni kwamba hata wilaya nyingine za mkoa huu kuna vitendo hivyo. Tushirikiane kuvitokomeza," alisema Kamanda Mbunda.

# Knauf yasaidia madawati, maji, taulo za kike Kilwa

Na Mwandishi Wetu

Kampuni ya Knauf Gypsum Tanzania Limited leo imekabidhi kisima cha maji kwa wakazi wa Kijiji cha Makangaga na kutoa madawati 200 kwa shule za msingi Makangaga na Kiranjeranje zilizopo wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi.

Kampuni hiyo pia imetoa katoni 16 za pedi za keki kwa Shule ya Sekondari Kiranjeranje, msaada ambao utasaidia kupunguza utoro kwa wanafunzi wa kike ambao hushindwa kuhudhuria masomo wanapokuwa katika mzunguko wa hedhi. Kisima kilichokabidhiwa kina uwezo wa kuhudumia zaidi ya watu 2,000 na kinatarajiwa kutatua changamoto ya ukosefu wa majisafi na salama ambayo ilikuwa inawakabili wakazi wa Makangaga waliolazimika kutembea umbali mrefu kutafuta huduma hiyo muhimu.

Akizungumza wakati wa kukabidhi misaada hiyo, Mkurugenzi wa Knauf kwa Kanda ya Afrika Mashariki, Lise Boshoff, alisema kampuni hiyo ambayo ina migodi ya kuchimba gypsum katika vijiji husika imeamua kutoa misaada kwa wakazi wa vijiji hivyo ikiwa ni sehemu ya kurudisha kwa jamii.

"Mradi huu wa maji siyo tu utaboresha afya za wakazi wa Makangaga bali pia utasaidia shughuli za uzalishaji mali, haswa kwa wanawake na wasichana ambao wanatumia muda mrefu kwenda kutafuta maji na badala yake wasichana watapata muda wa kuhudhuria masomo yao na wanawake kufanya shughuli mbali mbali za kiuchumi," alisema.

Kwa upande wa msaada wa madawati alisema ni sehemu ya jitihada za kampuni hiyo kuaidia kuboresha mazingira ya kujifunzia katika shule hizo mbili

"Tumeamua kutoa msaada wa madawati kwa kuwa tunajua umuhimu wa elimu kwa maendeleo. Kupitia madawati haya tunaamini kuwa wanafunzi wataweza kujifunza katika mazingira bora zaidi,"

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Eston Ngilangwa, aliishukuru kampuni ya Knauf kwa misaada hiyo na kusema msaada wa madawati umekuja wakati muafaka kwa kuwa shule zilizonufaika zilikuwa zinakabiliwa na uhaba wa madawati.

Kuhusiana na mradi wa maji, alisema maji ni uhai, na kuishukuru Knauf kwa kuwapelekea uhai. "Wakina mama na wasichana ambao walikuwa na mzigo wa kutafuta maji kwa ajili ya familia sasa watapata huduma hii muhimu jirani na maeneo wanayoishi," alisema.




Mkurugenzi wa kampuni ya Knauf Gypsum Tanzania Ltd Kanda ya Afrika Mashariki, Ilse Boshoff (kulia), akimsiliza Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi Kiranjeranje, Elibariki Kulilinda (kushoto), kabla ya kukabidhi msaada wa madawati 100 kwa shule hiyo, Wilayani Kilwa, mkoani Lindi jana. Kampuni hiyo pia ilitoa madawati 100 kwa shule ya msingi Makangaga, kisima cha maji katika Kijiji cha Makangaga na pedi za kike katoni 16 kwa shule ya sekondari Kiranjeranje. Katikati ni Meneja Rasilimali watu wa kampuni hiyo, Rose Mero. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi, walezi wapewa wito kuwarejesha watoto shuleni

Na Salome Mwasamale

WAZAZI na walezi nchini wametakiwa kushirikiana na serikali, kufanikisha kuwarejesha shuleni wanafunzi waliokumbwa na vikwazo kadhaa, ikiwamo kufeli mitihani ama kupata ujauzito, kuendelea na elimu ya sekondari.

Mratibu Elimu Kata ya Mbezi, mkoani Dar es Salaam, Suzan Masawe aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wananchi wa kata hiyo, kwenye mkutano wa kwanza mwaka huu, ulioandaliwa na diwani wa kata hiyo, Ismail Malata. Masawe alisema serikali inaamini baadhi ya watoto waliofeli ni kwa bahati mbaya kutokana na sababu mbalimbali za kifamilia, hivyo wakipewa nafasi nyingine wanaweza kufanya vizuri masomoni na kutimiza ndoto zao.

"Wazazi tusiipoteze nafasi hii muhimu kabisa iliyotolewa na serikali tuwatie moyo watoto wetu na kuwarudisha shuleni, ili kuitumia fursa hii adhimu ambayo imetolewa na mama yetu na rais wetu mpendwa Samia Suluhu Hassan," alisema Massawe.

Aidha aliiomba serikali na wananchi kwa ujumla kuungana na kuondoa vikwazo vya umbali kwa watoto ikiwamo kero ya usafiri, kwa kujenga shule za bweni, kutakakoongeza kasi ya ufaulu kwa wanafunzi.

Pia aliitaja changamoto ya ongezeko la uandikishaji watoto inavyoleta mlundikano wa wanafunzi, hivyo ujenzi wa shule unahitajika na kuwataka wananchi kutenga maeneo mengi zaidi kwa ajili ya ujenzi wa shule.

Diwani wa Kata ya Mbezi, Ismail Malata aliwataka wazazi na walezi kufuatilia kwa karibu maendeleo ya watoto wao ili kuondoa changamoto ya mimba za utotoni na ufaulu mbovu.

Pia, Malata aliahidi kutoa zawadi ya fedha taslimu kwa shule zitakazofanya vizuri ili kuongeza ufaulu, kwa kutoa zawadi kwa wanafunzi na walimu.

"Wazazi shirikianeni na walimu katika kufuatilia mienendo ya watoto wetu hii itasaidia kufanikisha kutokomeza ziro na kuongeza kiwango cha ufaulu katika kata yetu," alisema Mlata.

Alisema watoto wana tabia tatu ambazo lazima zifuatiliwe kwa kina tabia za nyumbani ambayo ni kazi ya wazazi na walezi, tabia za shuleni ambazo ni jukumu la walimu na tabia za nyumbani ambazo ni kazi ya kada zote tatu wazazi , walezi pamoja na walimu.

## TFS yagawa mamilioni miche

Na Friday Simbaya, MUFINDI

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kupitia Shamba la Miti Sao Hill mkoani Iringa katika kipindi cha miaka mitano cha kuanzia 2016/17 hadi 2020/21 Shamba la Sao Hill limezalisha na kugawa miche ipatayo milioni tano yenye thamani ya zaidi shilingi bilioni 1.5 kwa wananchi.

Katika msimu huu shamba litagawa miche ya miti milioni moja kwa taasisi za serikali, wananchi na watu binafsi ili kusaidia jitihadi za serikali za kupanda miti pamoja na kupunguza umasikini wa kipato kwa wananchi.

Hayo yalibainishwa jana na Meneja wa Shamba la Sao , Lucas Sabida, wakati wa uzinduzi wa ugawaji miti kwa taasisi za serikali, wananchi na watu binafsi wanaozunguka shamba hilo, kwa lengo la kudumisha ujirani mwema pamoja na kusaidia kulinda shamba hilo kutokana na majanga ya moto.

Alisema wamegawa miche ya miti milioni moja yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 300 kwa wananchi wanaozunguka shamba hilo, ikihusisha taasisi mbalimbali za serikali pamoja na watu binafsi.

Zoezi la ugawaji wa miti lilizinduliwa na Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Saad Mtambule, katika tarafa ya kwanza ya Ilundi na shamba hilo ambalo lina bustani tatu za kuzalishia miche ya miti ya misindano (pine) na mikaratusi ikiwemo Usokami na Mgololo wilayani Mufindi.

Shamba la miti sao hill ni miongoni mwa mashamba 23 ya miti ya kupandwa linalosimiwa na TFS na sehemu kubwa la shamba hilo lipo Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa wakati eneo dogo lipo wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro.

## Madarasa shida kwa shule Lindi

Na, Said Hamdani, LINDI

PAMOJA na Serikali kufanya juhudi ya kuboresha miundombinu ya elimu, Shule ya Msingi Matimba,Tarafa ya Nangaru, Mkoani Lindi, inakabiliwa na changamoto ya vyumba, vya madarasa, hali inayowalazimu wanafunzi kutumia chumba kimoja.

Afisa Tarafa ya Nangaru, Abdallah Chihoka aliyaeleza hayo kwenye kikao cha baraza la madiwani.

Chihoka akiwasilisha changamoto hiyo, alisema Shule hiyo ina wanafunzi 249 wasichana (138) na wavulana (111) ina vyumba vitatu vilivyokamilika,huku viwili vimejengwa kwa nguvu za wananchi.

Alisema ina wanafunzi kuanzia darasa la kwanza hadi la saba, vyumba viwili vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi bado kukamilika ujenzi wake,na umefikia hatua ya lenta vikisubiri kukamilishwa.

"Mh,mwenyekiti wanafunzi wa darasa la pili , tatu, nne na tano na la sita na saba wanatumia chumba kimoja kwa kupeana mgongo," alisema Chihoka.

Alisema kutokana na hali hiyo,kunakuwa na mwingiliano
mkubwa wakati wa masomo.



Ukurasa 12

**Miradi iliyomkwaza Rais Mara inapobeba sifa kupewa ukomo**



Ukurasa 13

CCM baada ya miaka 45, yajayo yafurahishe zaidi





Ukurasa 14

**CHOKOCHOKO UKRAINE VS RUSSIA**

**Ufaransa yaingia kuepusha vita, EU yaandaa mkeka wa vikwazo**


siasa

JUMATANO FEBRUARI 23, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


# Yalikoanzia mageuzi ya kisiasa

- Waliohama CCM walivyojitosa kimasomaso kuyafadhili
- Mmoja wao sasa ajutia kupoteza mali na wakati wake

**Na Sabato Kasika**

SASA ni takribani miaka 30 tangu kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi nchini mwaka 1992, lakini ujio huo ukiwa umetanguliwa na vuguvugu la mageuzi ya kisiasa lililoanza tangu 1989 kwa mijadala ya wazi na mingine ya kificho.

Baadaye mwaka 1991, vuguvugu hilo, lilihitimishwa kwa kongamano la mageuzi ya kisiasa likiwa na maazimio kadhaa, miongoni mwake ikiwa ni kuundwa kwa Kamati ya Kuratibu Mageuzi ya Kisiasa na Kikatiba (National Committee for Constitutional Reform - NCCR).

Mageuzi ya kisiasa nchini, hayawezi kukamilika bila kuwataja baadhi ya waasisi au mashujaa wake ambao wametoa mchango mkubwa, lakini pia wale ambao walijitolea kutoa mali zao ili kuyafanikisha na kutaka Tanzania iwe na demokrasia zaidi na upeo mkubwa wa kuyapambanua na kuyatafakari masuala ya kisiasa.


Katika mazungumzo yake na gazeti hili hivi karibuni jijini Dar es Salaam, mwanasiasa Hamad Thao, aliyewahi kuwa Naibu Katibu Mkuu wa TLP au Chama cha Labour, anaelezea jinsi Kamati ya Kuratibu Mageuzi ya Kisiasa na Kikatiba , ilivyofanya shughuli zake Tanzania Bara ikiwa chini Mwenyekiti wake Chifu Abdalah Fundikira, Wakili Mabere Marando akiwa Katibu, huku Zanzibar kukiwa na Kamati Huru ya Mageuzi (KAMAHURU), iliyoongozwa na Shaaban Mloo.

"Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo walikuwa ni Mchungaji Christopher Mtikila, James Mapalala, Mashaka Chimoto, Ndimara Tegambwage, Dk. Ringo Tenga na Balozi Kasanga Tumbo, "anasema Thao.

Anataja wajumbe wengine walikuwa ni Kasela Bantu, Prince Bagenda, huku baadhi ya vijana waliokuwapo wakati huo wakiwa ni James Mbatia, Anthony Komu, Idrisa Al-Nuru na Japhet Hassunga.

Anasema waanzilishi walikuwa ni wengi na kwamba baadhi wameshaaga dunia akiwataja Oscar Kambona, Fundikira, Mapalala, Mtikila, Chimoto, Tumbo, Kasela Bantu, Mloo, Maalium Seif na Bob Makani.

"Mageuzi ya kisiasa hayawezi kukamilika bila kuwataja wanasiasa hao ambao wengi wao kwa sasa ni marehemu, lakini wana mchango mkubwa katika harakati za kuwapo kwa vyama vingi nchini," anasema Thao.



Hamad Thao, akiwa kwenye harakati za kisiasa ACT- Wazalendo. **PICHA: MTANDAO**

**KAMATI KUYUMBA**

Anasema, NCCR hakikuwa chama bali ulikuwa ni mwamvuli uliowakutanisha wanaharakati wote waliokuwa wanataka nchi kurejea kwenye mfumo wa vyama vingi, lakini baadaye wanaharakati hao wakasambaratika.

"Kwanza makao makuu ya NCCR yalikuwa Magomeni Mikumi nyumbani kwa Chifu Fundikira, lakini baadaye ikatokea sintofahamu ndani ya kamati hiyo ndipo Fundikira akajiondoa na kuanzisha chama cha UMD," anasema Thao.

Anaongeza kuwa ilikuwa ni mwishoni mwa mwaka 1991, na kwamba Balozi Kassanga Tumbo, Kasela Bantu na baadhi ya wazee waliokuwa katika kamati hiyo waliondoka NCCR na kujiunga UMD.

"Huo ulikuwa ni mwanzo wa kusambaratika kwa kamati hiyo, huku Emmanuel Makaidi naye akaondoka na kuanzisha chama cha NLD, Edwin Mtei akaanziswha CHADEMA, Mchungaji Mtikila DP," anasema.

Thao anamtaja mwanasiasa mwingine kuwa ni Dastan Lifa Chipaka aliyekuwa akimwakilisha Oscar Kambona ambaye naye aliondoka na kwenda kuanzisha chama cha TADEA.

"Baada ya vigogo hao, kuondoka, ofisi za NCCR zikahamia nyumbani kwa Prince Bagenda mtaa wa Mtendani, ambapo akina Marando, Tegambwage, Mashaka Chimoto na wengine waliendelea na harakati za kisiasa," anasema.

Anasema, wanasiasa hao walijipanga upya na kugeuza kamati hiyo kuwa chama cha siasa na kukiita NCCR- Mageuzi na kwamba Marando alichaguliwa kuwa Mwenyekiti huku Bagenda akiwa Katibu Mkuu.

Tegambwage alichaguliwa kuwa Katibu Mwenezi, ambapo ofisi za makao makuu ya chama hicho, yalikuwa Kariakoo eneo la Mchikichini lakini baadaye yakahamia Manzese Argentina.

**MAMBO YA KUKUMBUKWA**

Thao anasema, miongoni mwa matukio ambayo hatayasahau, ni kitendo cha aliyekuwa Mwenyekiti wa chama chake cha TLP, Leo Lwekwama, kusigina Katiba ya Tanzania hadharani kutokana na kukerwa na

**INAENDELEA UK. 13**

# Miradi iliyomkwaza Rais Mara inapobeba sifa kupewa ukomo



Sehemu ya maadhimisho ya miaka 45 ya CCM yaliyofanyika Uwanja wa Karume mkoani Mara. **PICHA: MTANDAO**

**Na Richard Makore,** MWANZA

RAIS Samia Suluhu Hassan amekanyaga ardhi ya Mara katika ziara ya kichama, lakini pia ya kiserikali ambayo pamoja na kukata keki ya Jubilii ya miaka 45 ya CCM, anakutana na viporo vya miradi ya maendeleo, vilivyoanza lakini vimelala kwa miaka karibu 50 sasa .

Baada ya kukata keki ya miaka 45 na kulizuru kaburi la Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, Rais Samia hakuondoka bila kukagua miradi ya maendeleo iliyoko wilaya za Musoma, Butiama na Bunda.

Februari 7 mchana alipohitimisha ziara yake kwa kuweka jiwe la msingi kwenye mradi wa maji wa Nyabiho wenye thamani ya Shilingi bilioni.10.6 , ndipo anapokutana na taarifa nyingi kuhusu miradi mbalimbali iliyotelekezwa, ambayo licha ya kuanza kwa muda kukamilika kwake ni kitendawili.

Jambo hilo linamkera Rais Samia, kwa mfano Hospitali ya Rufaa ya Kwangwa iliyopo Musoma Vijijini imejengwa kwa takribani miaka 45, inashangaza na kuongeza maswali mengi.

Hospitali hiyo ilianza kujengwa wakati wa awamu ya kwanza na kupita awamu nne lakini hadi sasa haijakamilika, miradi mingine inayosuasua ujenzi wake ni pamoja na barabara inayotoka Musoma kupitia Makutano Ziroziro, Bukabwa, Kiagata, Sirori Simba, Remungorori, Ring'wani hadi Mugumu mjini.

Barabara hiyo inayojengwa kiwango cha lami imechukua miaka mingi bila kumalizika licha ya kuwa kiunganishi muhimu na makao makuu ya Wilaya ya Serengeti yaliyopo Mugumu lakini pia ikiendelea hadi mkoani Arusha.

Njia hiyo ilitegemewa kuwa kwa kujengwa kiwango cha lami hadi Mugumu ingekuwa mkombozi kwa wadau wengi lakini pia kwa watalii wanaotoka hifadhi za Ngorongoro na Serengeti kwenda Musoma pamoja na Mwanza.

> “ Moja wa makada wa CCM waliopata fursa ya kuzungumza na Rais, akiwa mkoani Mara ni Steven Wassira, aliyewasilisha kile kinachoonekana kama mahitaji ya wana Mara.

Hata hivyo, barabara hiyo muhimu kwa ajili ya kukuza utalii imechukua miaka minne sasa. Siyo hiyo pekee kuna nyingine kutoka Bunda kupitia ,Mgeta, Nata hadi Mugumu ambayo nayo ujenzi wake umechukua miaka mingi bila kukamilika.

Eneo lingine ni barabara ya kutoka Tarime kupitia Nyamongo hadi Mugumu ambayo nayo ujenzi wake unasuasua , barabara zote hizo ni muhimu katika kukuza utalii kutoka hifadhi za Serengeti mkoani Mara na Ngorongoro mkoani Arusha.

Kadhalika, barabara hizo zikijengwa na kukamilika kwa kiwango cha lami, zitafanikisha kusafirisha mazao ya chakula, biashara pamoja na mifugo kutoka Serengeti kwenda mikoa mingine.

Licha ya miradi kuanza na kutoa matumaini mapya kwa wananchi wa wa Mara tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama nalo ni donda ndugu.

Kutoka Musoma mjini ni takribani kilimita 90 kufika Muguu ambayo ni makao makuu ya Wilaya ya Serengeti, lakini vijiji zaidi ya 70 wilayani humo havina maji safi ya kunywa.

Ni miongoni mwa maeneo ya wilaya ambazo wananchi wake wanatumia maji ya visima vya asili na mito, lakini hakuna maji ya bomba kutoka chanzo cha uhakika licha ya mkoa wa Mara kupakana na Ziwa Victoria kwa sehemu kubwa pamoja na Mto Mara unaomwaga maji yake ziwani humo.

Vyanzo vyote hivyo vinaweza kusambaza maji katika Wilaya ya Serengeti kwa sehemu kubwa pamoja na Butiama na Musoma Vijijini.

**AWAPA MAJUKUMU**

Kutokana na miradi hiyo kusuasua, Rais anatoa maagizo mbalimbali kwa Mkuu wa mkoa na Mkuu wa wilaya pamoja na wabunge kuhakikisha wanasimamia suala hilo.

Anaiagiza pia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuanza kuchunguza miradi hiyo isiyokamilika kwa wakati na kutoa majibu sahihi kwa serikali.

Aidha, Rais anasema Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG), inapofanya ukaguzi kila mwaka inatoa mapendekezo kwa serikali kwa miradi isiyokamilika hivyo, TAKUKURU wahakikishe wanafanya kazi yao bila kusubiri kuagizwa.

Aidha, anaagiza wabunge, madiwani, mameya na wenyeviti wa halmashauri mkoani Mara kusimamia fedha za miradi hiyo ili iweze kukamilika kwa wakati.

Katika hilo, Rais Samia ametishia kuwashitaki kwa kuwatangaza madiwani na wabunge ambao hawasimamii miradi ya wananchi ili wapigakura wasiwachague nyakati za uchaguzi na kuwahimiza kuwa wachapakazi. Moja wa makada wa CCM waliopata fursa ya kuzungumza na Rais, akiwa mkoani Mara ni Steven Wassira, aliyewasilisha kile kinachoonekana kama mahitaji ya wana Mara.

Baada ya kusimama, Wasira akamkumbusha Rais Samia kwamba kwenye Ilani ya CCM ya 2022, chama kilichompa uhalali wa kuongoza kimetaja mradi wa ujenzi wa bandari ya Musoma itakayounganishwa na reli kutoka Tanga.

Anasema jambo hilo siyo tu kwamba halijatekelezwa bali halizungumzwi popote na huenda hata kwenye makabrasha ya Mwenyekiti Taifa limefutwa.

Wasira anamkumbusha Rais ambaye ni Mwenyekiti wa CCM kwamba tatizo la miradi ya maendeleo kusuasua mkoani Mara ni kubwa.

"Kumbe mnagombea bandari ya Bagamoyo ijengwe au isijengwe wakati hata kwenye ilani haipo lakini ya Musoma ambayo ipo kwenye ilani mmekaa nayo kimya wakati huo ni mkataba wa wapiga kura na watawala?" Anahoji.

Anauliza kwa nini msiwape hao Wachina hapa Mara wajenge bandari hii ambayo itakuwa kiunganishi cha Afrika Mashariki, mji wa Kisumu nchini Kenya na Jinja Uganda huku ikipokea mzigo kutoka bandari ya Mwanza kunusuru barabara zetu kutokana na shehena za malori ?

Mkongwe huyo wa siasa anahoji pia ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ambacho kimekwama kujengwa miaka kadhaa hadi leo, japo majibu yake hayakutolewa wakati wa ziara hiyo.

Lakini jambo la tatu ambalo ni muhimu kwa mahitaji ya watu wa Bunda anasema ni ugawaji upya wa mipaka ya mji wa Bunda na Halmashauri ya Bunda vijijini anasema ili wananchi wa eneo la Mugeta waende kwenye ofisi za halmashauri yao lazima wakatishe kilomita kadhaa za mji wa Bunda ili wafike Kibara.

Licha ya kwamba hawakuzungumza na Rais kama alivyopewa nafasi Wasira, wengine wanaona kuwa wanasiasa walifanya makosa kugawa mji wa Bunda kama yai na kiini chake, ikimaanisha mji ukawa katikati badala ya kutenganisha vipande viwili kama lengo lilikuwa kuleta huduma za jamii karibu na wananchi.

Makosa kama hayo yaliwahi kufanyika Musoma Vijijini na Mjini ambako licha ya kutenganishwa bado ofisi zilibaki mjini. Hata sasa makosa kama hayo yanaonekana kwenye Mji wa Tarime na halmshauri yake.

Kama lengo ni kuleta huduma za kijamii karibu na wananchi kwanini hilo halikuzingatiwa wakati wa kuweka mipaka? Bunda ni mfano mbaya kwa ugawaji wa halmashauri na madai ya baadhi ya wananchi, wanaona kwamba ili kuleta usawa mji wa Bunda ufutwe na kisha ziundwe halmashauri mbili zinazojitegemea ndani ya wilaya moja kama ilivyo Chalinze na Bagamoyo mkoani Pwani.

Wenyeji wanasema kwa kuwa Halmashauri ya Bunda Vijijini bado inasuasua ujenzi wa ofisi zake huko Kibara, waachane na suala hilo badala yake warudi kutumia ofisi zilizokuwa zinatumika zamani kabla halmashauri hiyo haijagawanywa kwa sababu hazina tija.

# CCM baada ya miaka 45, yajayo yafurahishe zaidi

**Na Deogratias Mutungi**

CCM inapokomaa na kutimiza miaka 45, ukweli ni kwamba kazi haiishii hapo , jukumu kubwa linaloanza rasmi ni kuendelea kubeba wajibu wa kuwalinda na kuwatunza Watanzania kwa kuwahakikishia amani.

Ni ukweli usiopingika kuwa amani inatunzwa na kulindwa haitoki peponi na hilo CCM imelitambua na kulifanyia kazi kwa miongo yote ya uhai wake hadi ilipokata keki ya miaka 45.

Kama chama kimekuwa na wakati mgumu tena kuna kipindi kimenyooshewa vidole na baadhi ya Watanzania wa ndani na nje ya mipaka kuwa ni chama kilichoshindwa kuendesha dola na kuwapa kile wanachotaka.

Mashambulizi ya udhaifu yalishika hatamu wakati wa awamu zote lakini zaidi mwaka 2008 chama kilipokuja na kauli mbiu ya "kujivua gamba."

Aidha, lawama zimeendelea kuwepo hadi sasa, hata hivyo, kisiasa duniani hakuna chama kilichopo madarakani kilicho salama dhidi ya mashambulizi ya kutoridhishwa na utawala, sera na falsafa za kiuongozi kutoka kwa raia na wapinzani wake.

Katika ulingo wa siasa zenye mfumo, aidha wa chama kimoja au vyama vingi huwezi kumridhisha kila raia, hivyo ni vigumu kukwepa lawama kwa namna yoyote ile hatamu ya usukani wa dola inapokuwa mikononi mwa chama chochote kile.



Naibu Katibu Mkuu wa CCM ( Bara) Christina Mndeme, mwanamama wa kwanza kushika wadhifa huo , hatua inayoakisi usawa wa kijinsia na ushirikishwaji. **PICHA: MTANDAO**

**KUBEBA AMANI**

Kwa kutumia uhuru wa katiba na demokrasia Watanzania wanaishambulia CCM kadri wanavyoweza lakini linapokuja suala la kuipa sifa CCM na serikali yake kwa kulifikisha taifa umoja, kuisifu na kuipongeza hakukwepeki.

Kuna upungufu ndani ya mfumo wa chama katika kusimamia na kuendesha dola kwa vile viongozi wa CCM ni binadamu na sio malaika hivyo makosa hayatakosekana.

CCM imefanikiwa kujenga falsafa ya umoja wa kitaifa na kuhimiza uzalendo kwa Watanzania, inayojaa amani na uzalendo chama kikiisimamia kupitia dola, kwa mantiki kuwa ndicho chama dola chenye wajibu wa kulinda amani na haki kwa wote.

Aidha, katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, Tanzania ni kioo cha dhahabu katika kulinda amani, umoja na uzalendo, hata hivyo si kwa ukanda huu pekee bali kwa Afrika kwani ni taifa lenye heshima ya pekee, ikilinganishwa na nchi nyingine barani humo.

Katibu Mkuu wa zamani wa Umoja wa Mataifa na mshindi wa Tuzo ya Nobel, Kofi Annan, aliwahi kuisifia Tanzania chini ya serikali ya CCM kuwa taifa lenye upekee wa amani ndani ya Afrika.

Hapa Afrika vyama vingi vya kisiasa vimekosa dira ya kuhifadhi amani na utulivu ndani ya mataifa yao na hivyo kuwa na chuki na ukiukwaji wa haki za binadamu kwa wananchi wao vitendo ambavyo hupelekea nchi kuwa wakimbizi nje ya mipaka ya mataifa yao.

> "Kofi Annan, aliwahi kuisifia Tanzania chini ya CCM kuwa taifa lenye upekee wa amani ndani ya Afrika.

Ipo mifano ya wazi kwa mataifa kama Rwanda, Burundi, Nigeria, Sudan na Sudan Kusini, Somalia na Congo DRC hakuna amani tangu uhuru lakini kwa Tanzania chini ya CCM imekuwa ni tofauti na mataifa hayo.

Aidha, amani ndiyo tunu ya maisha ya mwanadamu yaliposimama, bila amani dunia haiko sawa, Mwandishi wa kitabu cha "Ufilosofi wa amani na uzima wa umma" aitwaye David Swanson anaelezea kwa kina umuhimu wa amani katika ulimwengu huu ambao binadamu wanaishi na kuna viumbe vingine juu angani na chini ya ardhi.

Muktadha wa mwandishi Swanson katika kitabu chake cha amani kinaunganishwa na mantiki ya CCM kutambua thamani ya amani kwa raia wake na hivyo kuivusha hadi sasa inapojivunia kuwa taifa la mfano kwa Afrika na duniani kote ni la kipekee.

Chama Cha Mapinduzi kimekuwa na jitihada zake za kuendelea kuisimamia na kuilinda amani ya taifa hili ndani ya uhai wake wa miaka 45, hivyo ni wajibu wake kuitetea na kuilinda ili iendelee kwa miaka yote kwa maendeleo na ustawi wa taifa, bila kujali kitakuwa na wakati gani au kitakuwa wapi katika miaka mingine mingi ijayo.

Amani ni tunda la uhimilivu na ukomavu wa uchumi. Ndiko kuliko na uhuru wa kuabudu, kuzalisha mali, kujiamulia la kufanya kwa mujibu wa sheria na ndiyo nguzo ya demokrasia.

Kinacholeta maendeleo popote ni uwepo wa amani kwa vile hapo ndipo wananchi wanapoweza kuweka vitega uchumi, kuzalisha na kuuza bidhaa mbalimbali na ukawa mwanzo kukua uchumi wa taifa.

***Maoni: dmutungid@yahoo.com, 0717718619***

# Yalikoanzia mageuzi ya kisiasa

**INATOKA UK. 11**

na kile kilichomo ndani yake.

"Ilikuwa ni mwaka 1996 kwenye viwanja vya Jangwani Dar es Salaam, kulikuwa na mkutano mkubwa uliotishwa na vyama vya upinzani, ilipofika zamu yake kuhutubia, alichukua katiba na kuisigina," anakumbusha.

Kwa nini? Thao anasema, sababu kubwa ya Lwekamwa kufanya hivyo, alikuwa akiamini kuwa katiba hiyo si ya Watanzania, bali ni CCM, kwa kuwa kwa nje ilikuwa na rangi ya kijani.

"Kitendo hicho kilisababisha awekwe ndani kwa miezi mitatu bila dhamana, lakini baadaye akadhaminiwa, kesi ikaendeshwa kwa mwaka mmoja, lakini baadaye serikali ikasema haina haja ya kuendelea na kesi hiyo," anasema.

Anasema, huenda Lwekamwa kufanya kitendo hicho, ilichangia kuifanya serikali kubadili rangi ya katiba na kuwa ya zambarau, na kwamba inawezekana ilibaini kuwa mwanasiasa huyo alikuwa na sababu za msingi.

**KUGHARAMIA MAGEUZI**

Wanapotajwa vinara na wafadhili wa mageuzi ya kisiasa nchini, Thomas Ngawaiya, hawezi kusahaulika. Ni miongoni mwao kwa kuwa alitoa jengo lake la ghorofa kuwa makao makuu ya vyama vya upinzani kwa miaka nane.

Akiwa na ari ya kuwa mwanamageuzi alikuwa mbunge wa Moshi Vijijini NCCR-Mageuzi baada ya uchaguzi wa mwaka 2000 hadi 2005 aliposhindwa , na katika ufafanuzi wake, Ngawaiya anasema, anaumia kupoteza muda na mali zake bure kwa upinzani ambao haukuwa na nia ya kweli hasa baada ya kuhama CCM ili kumuunga mkono Augustine Mrema, aliyejiunga na NCCR-Mageuzi miezi michache kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 1995.

"Baada ya kuhamia huko, nilitoa magari na mali nyingine ili kufanikisha ushindi kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 1995 na kisha nikatoa sehemu ya ghorofa ya kwanza na pili kuwa ofisi ya NCCR-Mageuzi," anakumbusha.

Anafafanua kuwa chama hicho kililitumia jengo hilo kuanzia mwaka 1996 hadi 1999, Mrema alipohamia TLP, na kwamba mabadiliko hayo yalisababisha ofisi zilizokuwa zikitumiwa na NCCR-Mageuzi kuwa za chama cha TLP.

"Ofisi zaligeuzwa kuwa za TLP kwa sababu nilienedelea kuwa na Mrema hadi mwaka 2006 nilipoamua kurudi CCM, lakini kwa miaka yote hiyo nane nilitoa jengo langu litumike bure kwa vyama vya upinzani," anasema.

Kada huyo anasema, uamuzi wake wa kurudi CCM ulitokana na kile anachodai kubaini kutokuwapo kwa upinzani wa kweli, na kwamba hakuona kwa nini aendelea kubaki kwa watu wanaoigiza.

"Nilijitolea kutoa mali za bure na kwani kama ningepangisha vyumba vya ghorofa langu, ningelipwa fedha nyingi, lakini sikufanya hivyo kwa lengo la kuimarisha mageuzi. Sina hamu tena na upinzani," anasema.

JUKWAA LA VIONGOZI

CHOKOCHOKO UKRAINE VS RUSSIA

# Rais Macron aingilia kuepusha vita vya wababe Biden, Putin

• EU yaandaa mkeka wa vikwazo 'mambo yakae sawa'



Marais Joseph Biden wa Marekani (kushoto) na Vladimir Putin wa Russia, wahusika wakuu wa mgogoro wa Ukraine unaotajwa kuwa kitisho cha vita vya tatu vya dunia. **PICHA: AFP**

**Na Gaudensia Mngumi**

UKRAINE iliyo katikati ya mzozo wa kidiplomasia na hata kitisho cha vita, ikitishiwa kuvamiwa upande mmoja na Russia ambayo nayo itanyamazishwa na majeshi ya Kujihami ya Jumuiya ya Kujihami ya Magharibi (NATO), inatajwa kuwa taifa kubwa kuliko yote Ulaya likiwa na watu takriban milioni 43.

Taifa hilo linalozua mzozo wa Marekani na Russia, ilikuwa sehemu ya Jamhuri za Kisovieti ya Urusi (USSR) na historia inaeleza ilikuwa rasmi sehemu ya Jamhuri za Kisovieti ( Soviet Union) tangu 1922.

Ukraine imegawanyika katika jamii kuu mbili za watu wanaozungumza Kirusi ambao wanajiona ni sehemu ya Russia, pia wapo wengine wanaoongea 'Kiukraini', lakini lugha inayotawala ni Kirusi.

Ukraine ilikuwa na umuhimu wa kipekee kwa Russia na ndiyo njia yake kuu ya kusafirishia gesi asilia kupeleka Ulaya, kwa miaka kadhaa sasa.

Russia ikiwa ya pili kwa uzalishaji wa gesi asilia duniani baada ya Marekani, inasafirisha gesi yake kwenda Ulaya ikutumiwa kama nishati na pia kupasha mataifa hayo joto wakati wa msimu wa baridi na maanguko ya theluji.

> "Ukraine ilikuwa na umuhimu wa kipekee kwa Russia na ndiyo njia yake kuu ya kusafirishia gesi asilia kupeleka Ulaya, kwa miaka kadhaa sasa.

**KUIKOMOA RUSSIA?**

Kuna madai kuwa mzozo uko kiuchumi zaidi, kwa kuwa unalenga na kulitishia bomba la gesi la kampuni kubwa za gesi la Russian la Gazprom (GAZP.MM), ndilo linalotishiwa kulipuliwa na Marekani na NATO, iwapo itaivamia Ukraine kama itasaini kuwa mwanachama wa NATO.

Hapo awali Russia ilikuwa inasafirisha gesi kwenda Ulaya kupitia Ukraine lakini miaka ya karibuni inasafirisha nishati hiyo muhimu kwa mataifa ya Ulaya kupitia Poland.

Likiandika habari za mabadiliko hayo Shirika la Habari la Reuters la Uingereza liliripoti kuwa gesi hiyo sasa itakuwa inapitishiwa kwenye njia ya Polanda -Yamal- Europe Pipeline, Ukraine ikiwekwa pembeni.

Kutokana na umuhimu wa gesi kwa mataifa ya Ulaya hadi sasa hayajakubali moja kwa moja kuiwekea Russia vikwazo japo Ulaya inasema imeshaviandaa, lakini ikisisitiza juhudi za kidiplomasia ziendelee mchana na usiku kuitaka Russia kuondoa vikosi vyake vilivyoko kwenye mpaka wa Ukraine. Na sasa Ufaransa iko ulingoni.

**CHUMVI NA VIDONDA**

Kwa mujibu wa taarifa za televisheni ya ALJAZEERA, Rais Vladimir Putin wa Russia, anapuuza vitisho hivyo vya Marekani na kutoa maelekezo mapya ya kuwataka wanajeshi wake kuendelea kulinda na kutuliza amani kwenye majimbo ya Ukraine yaliyojitenga karibu ya Donetsk na Luhansk, pia anayatambua kuwa ni maeneo yenye uhuru kamili.

Akinukuliwa Jumatatu wiki hii Putin, anamtaka Waziri wa Ulinzi kutekeleza jukumu la ulinzi wa amani kwenye majimbo hayo ya Mashariki .

Wakati Russia ikiwaunga waasi wanaojitenga na Jamhuri ya Ukraine, Marekani kwa upande wake inaunga mkono ombi la Ukraine la kutaka kuwa na kikao cha haraka cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa , kujadili hali halisi ya Ukraine

Marekani kuunga mkono ombi la Ukraine kwa Umoja wa Mataifa inatokana na maelezo kuwa Russia kutambua na kuunga mkono majimbo mawili ya Ukraine yaliyojitenga ni kuchochea chokochoko nchini humo na kuingilia uhuru kamili wa taifa hilo na haki ya kujitawala.

Katika msimamo wake, Marekani inasema UN lazima iilazimishe Russia kuheshimu uhuru kamili wa taifa hilo na haki ya kujitawala ya Ukraine, ambayo ni mwanachama wake.

**JUHUDI ZA KARIBUNI**

Rais wa Marekani Joseph Biden na Putin wa Russia, wanategemewa kukutana kujadili mgogoro wa Russia na Ukraine, mkutano unaondaliwa na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macro .

Marais hao wameridhia kukutana katika hatua za mwisho za kidiplomasia kujaribu kuepusha uwezekano wa Urusi kuivamia Ukraine. Hata hivyo, Ikulu ya Russia siku zote imekuwa ikisema 'Putin yuko tayari kwa mazungumzo ya aina yoyote ile.'

Inaripotiwa mkutano kati ya viongozi hao unaandaliwa na Rais wa Ufaransa Macron aliyezungumza na pande zote mbili kwa njia ya simu. Ofisi ya Macron inasema Biden na Putin, wamekubaliana kukutana.

Baadaye pia wamekubaliana kukutana na pande zote husika katika mgogoro wa Ukraine na Russia, ili kujadili masuala muhimu ya usalama na uthabiti wa Ulaya. Ofisi hiyo inasema mkutano huo utafanyika kwa masharti ya Puttin kutoivamia Ukraine.

Msemaji wa Ikulu ya Marekani Jen Psaki, anasema nchi yake iko wazi katika suala hilo na kwamba wamejitolea kutumia diplomasia hadi pale uvamizi utakapofanyika akisema kwa sasa Russia inaonekana kuendelea kujitayarisha kuishambulia Ukraine.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Anthony Blinken, na mwenzake wa Russia, Sergei Lavrov, watakutana kesho kujadili ajenda za mkutano wa marais wao. Ikulu ya Urusi haijatoa maoni yoyote juu ya kukutana kwa Biden na Putin lakini siku zote imekuwa ikisema Putin yuko tayari kwa mazungumzo ya aina yoyote ile.

Mkutano huo unatoa matumaini ya kuzuwia uvamizi wa Urusi nchini Ukraine ambako maafisa wa Marekani wamesema huenda ukatokea wakati wowote kutokana na wanajeshi zaidi ya 150,000 wa Russia kujikusanya karibu na mpaka wa Ukraine

**EU YAANDAA VIKWAZO**

Wakati huohuo, Mkuu wa Sera za Kimataifa wa Umoja wa Ulaya (EU), Josep Borrell, amekaribisha hatua ya kufanyika mkutano wa kilele kati ya Putin na Biden lakini akaonya kuwa iwapo diplomasia itashindwa, umoja huo wenye wanachama 27, umeshakamilisha vikwazo itakavyowekewa Russia iwapo itaivamia Ukraine. Halmashauri ya Umoja wa Ulaya pia kupitia rais wake, Ursula von Der Leyen, inaeleza kuwa imetayarisha vikwazo vingine vitakavyoizuia Russia kufikia masoko ya kifedha vikwazo vinavyoulenga moja kwa moja uchumi wa taifa hilo.

Russia kwa upande wake imeendelea kukanusha mipango yoyote ya uvamizi huo na Msemaji wa Rais Putin, Dmitry Peskov, anasema haina haja ya kushambulia akiwataka washirika wake wa Magharibi kufikiria wanachokisema.

Peskov anasema kutokana na historia ya Russia haijawahi kumshambulia yoyote na Urusi iliyopitia vita vingi ni taifa ambalo haliwezi kutamka hata neno vita na katika hatua nyingine, Mawaziri wa UE walikutana Jumatatu jijini Brussels, kujadili mzozo huo kufuatia mashambulizi yaliyopamba moto katika eneo la Donbass mashariki mwa Ukraine, kati ya vikosi vya serikali na watu wanaotaka kujitenga wanaoungwa mkono na Russia.

• Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.



## Waipa kongole serikali fedha za ukarabati madarasa

Na Peter Mkwavila, DODOMA

Serikali imepongezwa kwa kutoa Sh.milioni 59, kwa ajili ya ukarabati wa vyumba sita vya madarasa kwenye Shule ya Msingi Chamwino 'A' jijini hapa, vinavyokuwa vinavuja maji msimu wa mvua na kusababisha wanafunzi kushindwa kusoma.

Wakazi wa kata ya Chamwino jijini hapa walitoa pongezi hizo jana mbele ya Naibu Meya wa Jiji la Dodoma Emmanuel Chibago, walipokuwa wakizungumza kwenye kikao cha mkutano wa hadhara wa kujadili maendeleo uliofanyika kwenye shule hiyo.

Mkazi wa eneo hilo, Asha Ramadhani alisema fedha hizo ambazo zimetolewa kupitia Halmashauri ya Jiji hilo zimesaidia kuondoa kero hiyo kwa wanafunzi na walimu.

"Fedha zilizotolewa na serikali kwa kupitia Jiji la Dodoma, zimekuwa mkombozi kwa wanafunzi na walimu ambao kwa kipindi kirefu wananyeshewa wanapokuwa kwenye madarasa hayo ambayo mabati yake ni machakavu, tuna kila sababu ya kumshukuru Rais kwa serikali kutoa fedha hizo za ukarabati,"alisema.

Naye, Mariam Hassani, alisema ukarabati huo ni chachu kwa walimu na wanafunzi katika kuongeza ufaulu.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata hiyo, Jumanne Ngede,aliomba wazazi na walezi kuiunga mkono serikali kutokana na juhudi kubwa zinazowekezwa kwenye elimu.

Naye Naibu Meya, Chibago aliagiza uongozi wa kata kuhakikisha ukarabati huo unaanza mara moja ili kutatua kero hiyo.

# Mchango wa TESP mazingira ufundishaji vyuoni waanikwa

Na Renatha Msungu, DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amesema kupitia Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu nchini (TESP), serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Ualimu ili kuongeza ubora wa elimu nchini. Prof. Mkenda alibainisha hayo juzi jijini hapa kwenye hafla ya ugawaji kompyuta 300 kwa vyuo vya ualimu awamu ya tatu zilizotolewa na Wizara kupitia mradi huo.

Alivitaja vyuo hivyo ni pamoja na Marangu, Kleruu, Vikindu, Patandi, Korogwe, Mpwapwa, Shinyanga, Ilonga, Tarime, Tandala, Butimba, Mtwara na Morogoro.

Alisema dhima ya Vyuo vya Ualimu nchini ni kuandaa walimu mahiri na wanaotosheleza mahitaji katika shule za Awali, Msingi na Sekondari.

"Kutokana na dhima hiyo, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika Vyuo vyote vya Ualimu vya Serikali nchini mkazo ukitolewa katika uboreshaji wa miundombinu, vifaa vya kujifunzia na kufundishia na matumizi ya TEHAMA kama nyenzo muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Uboreshaji huu unakwenda sanjari na maendeleo makubwa katika matumizi ya Sayansi na Teknolojia katika ufundishaji na Ujifunzaji,"alisema.

Hata hivyo, alisema Wizara inaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Vyuo mbalimbali nchini ikiwemo ukamilishaji wa Chuo cha Kabanga, Ujenzi wa vyuo vipya vya Sumbawanga, Dakawa, Mhonda na Ngorongoro unaendelea.

"Ukarabati na ujenzi wa baadhi ya miundombinu katika vyuo vya Morogoro, Mpwapwa, Tukuyu, Kasulu, Butimba na Patandi nao unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha 2021/2022. Hadi sasa Wizara imetoa mafunzo ya matumizi ya Tehama katika kufundishia na kujifunzia kwa wakufunzi wote 2,300 kutoka Vyuo vya Ualimu vya Serikali yote 35,"alisema.

Prof.Mkenda aliwaagiza wakuu wa vyuo hao kutunza Kompyuta hizo kwa kuwa zimenunuliwa kwa gharama kubwa na zitumike kwa maelngo yaliyokusudiwa.

"Kila Mkuu wa Chuo ahakikishe mali zote za Serikali zinatunzwa ipasavyo ili kuleta tija ya fedha zilizotumika na Vyuo vyote vya Ualimu vizingatie matumizi sahihi ya kompyuta hizi ikiwemo kuhaikikisha ziko katika mazingira yaliyo safi na salama kama ilivyo kanuni na taratibu za kutunza na kuhifadhi vitu vya TEHAMA,"alisema.

Awali, Naibu Waziri Omari Kipanga, alisema bado kuna ukosefu wa walimu nchini hivyo serikali inaendelea kukabiliana na hali hiyo ikiwamo kubadilisha mitaala ili kuendana na masuala ya teknolojia.

Kwa upande wake,Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia,Prof. Caroline Nombo, alisema mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Canada ambapo mchango wa Canada katika mradi huo ni jumla ya Dola za Canada milioni 53.

Alisema mchango wa Serikali ya Tanzania ni katika kugharamia shughuli mbalimbali za uendeshaji wa vyuo ikiwamo gharama za malipo ya chakula kwa wanachuo na mafunzo ya ualimu kwa vitendo.

Alibainisha hadi kufikia Desemba 2021 wastani wa utekelezaji wa malengo ya mradi ulikuwa ni asilimia 75.83.




Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago (katikati), akizungumza na wazazi/ walezi wa Kata ya Chamwino, katika mkutano wa kujadili maendeleo ya shule ya msingi Chamwino A, jijini humo juzi. Kulia ni Diwani wa kata hiyo, Jumanne Ngede. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mbinu kudhibiti uhalifu mtandaoni yatajwa

Na Augusta Njoji, DODOMA

NAIBU Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Andrea Kundo amesema kutokana na matukio ya uhalifu wa kimtandao kuongezeka ni vyema Jeshi la Polisi na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuwa na ujuzi na teknolojia ya kukabiliana nayo ili taarifa za nchi zisidukuliwe.

Kundo aliyasema hayo jijini hapa alipokuwa akifungua mafunzo ya usalama mtandaoni kwa ajili ya Jeshi hilo, ofisi hiyo na kamati ya wataalamu ambayo yanahusu upelelezi wa makosa ya kimtandao.

Alisema kwa kuwa dunia ya sasa imejawa na wahalifu wa mitandaoni na matukio ya aina hiyo yamekuwa yakiongezeka na kubuniwa mbinu mpya za kihalifu, hivyo wataalam nchini wanapaswa kuwa na ujuzi wa kukabiliana nayo.

"Serikali imeliona hilo hivyo kupitia Wizara hii katika kusimamia sera ya TEHAMA ya mwaka 2016 inayosisitiza matumizi salama ya mifumo na miundombinu ya TEHAMA pamoja na Sheria ya Usalama Mtandaoni iliunda kamati maalum ya kitaifa ya kukabiliana na uhalifu huu Machi mwaka 2021,"alisema.

Alisema mafunzo hayo ni mapendekezo ya kamati ili kukabiliana na hali hiyo na kuwataka washiriki kuzingatia ili kuimarika kwenye mapambano ya uhalifu wa mitandaoni.

"Niwaombe tu kwamba mzingatie yale ambayo mnakwenda kujifunza mkielewa kuwa tupo kwenye mapambano ya kimtandao ambayo tusipokuwa makini tutakuwa kila siku taarifa zetu zinadukuliwa na hivyo kuhatarisha usalama wa nchi,"alisema.

Vile vile, alisema uendeshaji wa kesi za uhalifu huo zitasababisha shida iwapo hawatazingatia mafunzo hayo na kutoa faida kwa wakosaji wa kimtandao kushinda kesi zao. Awali, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mashtaka ,Kamishna ,Msaidizi Mwandamizi wa Polisi(SACP), Deusdedit Nsimeki, alisema kumekuwa na malalamiko tangu kutoka kwa baadhi ya wananchi ambao wamekuwa na kesi ya kupotelewa na simu zao kulipia gharama kubwa tofauti na simu ambayo imepotea na hivyo kuharibu taswira ya jeshi na taaluma kwa ujumla.

"Mafunzo hayo yatasaidia kuongeza tija na uadilifu katika utendaji kazi wenu ikiwa ni pamoja na kupambana na uhalifu na kupelekea kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa,"alisema.

Kamishna wa Polisi Uchunguzi wa kisayansi (CP FB), Shabani Hiki, alisema mafunzo hayo yatapunguza lawama nyingi za wananchi kwa jeshi hilo.

Mafunzo ya kukabiliana na makosa ya uhalifu mtandaoni yanaendeshwa katika maeneo tofauti ya Dodoma, Dar es Salaam na Morogoro, ambapo wataalamu zaidi ya 400 wanapatiwa mafunzo yanayohusu upelelezi wa makosa ya kimtandao, ubobezi katika tathmini ya usalama wa mifumo na Sayansi ya kiuchunguzi katika mitandao,

Matumizi ya moduli ya uhalifu mtandao, uandaaji wa mwongozo wa upelelezi na uendeshaji wa mashtaka kwa mashauri ya kimtandao,



# Akamatwa tuhuma kukutwa na pombe zilizopigwa marufuku

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limemkamata Ruben Adam (26), mkazi wa Kitongoji cha Lubele kilichopo wilayani Kyela kwa tuhuma za kukutwa na pombe kali zilizopigwa marufuku kuingia nchini ambazo zinadaiwa kutoka Nchi jirani ya Malawi.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mbeya, Ulrich Matei alisema jana kuwa walimkamata mtuhumiwa baada ya kufanya msako kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Kyela.

Alizitaja pombe kali zilizokamatwa kuwa ni Ice Dry London Gin chupa 12 za 200ML,Rider 200ML chupa 28, A1 Gin chupa 24ML 200 na Right Choice chupa 28 za 200 ML.

"Hadi sasa mtuhumiwa yuko chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi na baada ya shauri lake kukamilika atafikishwa mahakamani kujibu tuhuma za kukutwa na pombe hizo,"alisema Matei.

Katika hatua nyingine Jeshi hilo limewakamata watuhumiwa 12 kwa makosa mbalimbali ikiwamo wizi wa mifugo, kuvunja nyumba na kuiba.

Matei alisema Februari 20, mwaka huu majira ya saa 11 alfajiri katika Kitongoji cha Kasama, wilayani Kyela, Sinael Mwalambilambota (36) aligundua ameibiwa ng'ombe wake dume, mwenye thamani ya Sh. 800,000.

Kutokana na tukio hilo, Jeshi la Polisi lilianza msako mara moja na kumkamata Maneno Seme(30) mkazi wa Kijiji cha Kasumulu akiwa katika harakati za kutafuta mteja ili kumuuza ng'ombe huyo.

Aidha Jeshi hilo pia linawashikilia watuhumiwa 11 kwa tuhuma za kuvunja nyumba za watu majira ya usiku na kuiba samani mbalimbali.

Kamanda Matei alisema watuhumiwa hao walikamatwa februari 20 baada ya kupata taarifa za siri kutoka kwa wasamaria wema juu ya uwapo wa wahalifu hao jijini Mbeya.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Victor Richard [39] Mkazi wa Makunguru, Justine Norbert (19), Geofrey Simon (20), Erick Matheo wakazi wa Makunguru, (27) mkazi wa Ilemi, Jonas Betram (32) ,Henry Mwamfupa (28) mkazi wa Mwanjelwa.

Wengine ni Robert Mwakyusa (36) mkazi wa Iyunga, Goodluck Frank (20)mkazi wa Nonde, Benny Fredy, (26) mkazi wa Nonde, Said Hamis (31) mkazi wa Iganzo na Abdallah Lucas (22) mkazi wa Ghana.

Alidai kuwa katika upekuzi uliofanywa na Jeshi la Polisi katika makazi ya watuhumiwa walikutwa wakiwa na mali mbalimbali za wizi kama vile Mtungi wa Gas Mihan, Jiko la Gesi aina ya Boss, Diaba moja , Godoro moja , Amplifier, Simu mbalimbali za mkononi nzima na mbovu, Computer mbili, Memory card, flash disk na subwoofer ambavyo viliibwa maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya.

Watuhumiwa wote walikiri kujihusisha na vitendovya uvunjaji na wizi na kwamba msako wa kuwatafuta watuhumiwa wengine ambao ni wapokeaji wa mali hizo unaendelea..



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, mkoani humo juzi, kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali ikiwamo sekta ya barabara, afya, elimu na ukusanyaji wa mapato kwa mwaka 2022. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Shule yachochea wafugaji kusoma

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

IMEELEZWA kuwa uwepo wa shule binafsi ya mchepuo wa Kiingereza ya Kelly's, iliyopo katika kijiji cha Nyang'uru Kata ya Mapogoro wilayani Mbarali, mkoani Mbeya, kumechochea jamii ya wakulima kuwekeza katika elimu na kupunguza kutumikishwa katika ufugaji.

Mkurugenzi wa Shule hiyo ,Kennedy Lutambi, alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na msukumo wa kuwekeza elimu wilayani humo kwa lengo la kusaidia serikali kusogeza huduma ya elimu karibu na wananchi.

"Nimelenga kuwekeza katika kijiji hiki kutokana na kuwapo kwa maono ya kusaidia suala la elimu kwa jamii iliyosahaulika na kuhamasisha umuhimu wa elimu kwa kizazi cha sasa na kijacho huku tukitoa kipaumbele pia kwa watoto wa makundi maalum kama walemavu ",alisema Lutambi.

Alisema kuwa uwekezaji katika elimu unahitaji kuungwa mkono na wakazi wa maeneo husika na kwamba tangu kuanzishwa kwa shule hiyo idadi ya wanafunzi imekuwa ikiongezeka na kufikia wanafunzi 377.

Licha ya uwekezaji huo lakini Lutambi aliiomba serikali kupunguza utitiri wa tozo mbalimbali na kukwamisha jitihada za utoaji elimu kwa ufanisi.

Aliiomba Serikali kuangalia mifumo mizuri ya Sera ya Elimu ambayo itakuwa wezeshi kwao kwa kupunguza utitiri wa tozo kutokana na mchango wao mkubwa katika Sekta ya elimu.

Mwalimu Mwanzilishi wa Shule Ayoub Kibona alisema kuwa kwa sasa wazazi wameelimika kwa kuwekeza kwenye masuala ya elimu kwa vijana na kwamba katika kuongeza ufanisi na ushirikiano mzuri wamechangia shughuli mbalimbali za kijamii hususani kuchangia madawati 300 kwenye Shule Msingi Mabadaga iliyoko wilayani Mbarali.

# Wataka miradi ujenzi kuzingatia wenye ulemavu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU wa elimu Jijini Mbeya wamewaomba wataalam wanaotekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kuhakikisha wanazingatia miundombinu ya watoto wenye ulemavu ili waweze kusoma kwa raha na kutimiza ndoto zao.

Kauli hiyo ilitolewa jana na mdau wa elimu mkoani Mbeya Thabitha Bugali, alipozungumza na Nipashe juu ya hali ya miundombinu ya elimu kwa watoto wenye ulemavu.

"Tulijaribu kutembelea baadhi ya shule za msingi vijijini tukabaini miundombinu ya shule hususani vyoo havisapoti watoto wenye ulemavu kupata huduma, tunaishukuru serikali kwa mwongozo mpya walioutoa kuhusu namna bora ya kujenga ikizingatia miundombinu ya watu wenye ulemavu," alisema Bughali.

Alisema kuwa kuna kila sababu serikali inapopata wahisani wa kuwekeza katika sekta ya elimu wajikite zaidi maeneo ya vijijini ili kuboresha miundombinu ya vyoo ili vikidhi mahitaji kwa kuzingatia watoto wenye ulemavu.

Jaqline Sanga mkazi wa Mbeya , alisema kuwa licha ya kuwapo kwa vikwazo mbalimbali vinavyowakabili watoto wenye ulemavu shuleni lakini jamii inapaswa kushirikiana na serikali kwa kutumia nguvu kazi katika kuboresha miundombinu ya vyoo, vyumba vya madarasa na si kuiachia jukumu hilo serikali pekee.

Mwenyekiti wa Chama cha Walemavu mkoa wa Mbeya, (Chawata), Jimmy Ambikile, alisema bado kuna tatizo kwenye suala la miundombinu kwa walemavu kuanzia shule za msingi hadi sekondari.

Vilevile alisema hata kwenye majengo ya taasisi mbalimbali za umma hakuna miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu hivyo suala hilo lifanyiwe kazi ili nao wapate huduma bila vikwazo.





# Serikali yasisitiza utoaji wa risiti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Jamal Kassim, amesema kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi Na. 7 ya mwaka 2009, kila mfanyabiashara anayefanya biashara Zanzibar anatakiwa kutoa risiti anapofanya mauzo.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kinachoendelea Chukwani, mjini Zanzibar wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Chakechake, Shaib Hassan Kaduara.

Kaduara alitaka kujua kuwa maduka makubwa (supermarket) na migahawa Zanzibar haitoi risiti za mauzo, je, ni utaratibu gani wa kukusanya mapato ya Serikali unaotumika kupitia 'supermarket' na migahawa hiyo.

Waziri Jamal alisema wafanyabiashara wa 'supermarket' pamoja na wa migahawa na wafanyabiashara wengine wote wanatikwa kwa mujibu wa sheria kutoa risiti wanapofanya mauzo ya bidhaa au huduma.Alisema kwa kufanya hivyo, ndipo serikali kupitia Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) hukusanya kodi stahiki kwa mauzo yaliyofanywa.

"Kama ziko 'supermarket' hazitoi risiti kwa mauzo yaliyofanywa ni makosa na wanapogundulika hutozwa faini pamoja na kulipishwa kodi waliyoikwepa," alisema.

Pia alisema kila mfanyabiashara anatakiwa kutoa risiti wakati anapofanya mauzo, hivyo kutokutoa risiti ni kosa.

Alisema serikali ya Zanzibar kwa kutambua uwepo wa sheria hiyo haijaruhusu wafanyabiashara wa 'supermarket' kutokutoa risiti na wanatakiwa kuendelea kutoa risiti kwa kutumia vitabu au kutumia mifumo yao ya mauzo ambayo wanaimiliki.

Waziri alisema kupitia mfumo mpya wa utoaji risiti wa VFMS, wafanyabiashara wa 'supermarket' na migahawa yote iliyoko Zanzibar watafungiwa mfumo wa VFMS na watatakiwa kutoa risiti kwa mfumo huo, ambapo nao watapatiwa vifaa ili watoe risiti za kielektroniki kupitia mfumo au mifumo yao kuunganishwa na mfumo wa VFMS.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Hospitali za Pemba zapungukiwa X- Ray

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya, Ustawi wa Jamii,Jinsia na Watoto imekiri kwamba hospitali za Pemba zilikuwa na upungufu mkubwa wa filamu za X- Ray kwa sababu ilikuwa nje ya uwezo wa wizara hiyo.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Konde, Zawadi Amour, aliyetaka kujua wizara inajipanga vipi kuhakikisha huduma ya X-Ray inapatikana Pemba.

Alisema wizara tayari imepata msambazaji wa filamu hizo na ziko za kutosha katika hospitali zote ambazo zinaweza kutumia zaidi ya miezi mitatu lakini pia wanatarajia kupokea filamu zingine.

Mazrui alisema wizara yake itaweka mashine za kisasa katika hospitali za Pemba hivi karibuni kupitia fedha za serikali na wadau wa maendeleo.

Pia alisema hospitali ambazo ujenzi wake unaendelea na utakamilika Juni, mwaka huu, zitafungwa mashine zenye teknolojia za kisasa na kidigitali za X-Ray ili kuondoa usumbufu wa huduma hizo kwa wananchi.

Hata hivyo, Waziri huyo alisema hospitali hazitoi dawa zilizoisha muda wa matumizi na wagonjwa wa kisukari hupewa dozi ya mwezi mmoja.

Alisema kuwa utaratibu uliowekwa ni kwamba dawa kutoka Stoo kwenda wodini ni lazima zisizidi miezi zaidi ya mitatu kabla kumaliza muda wa matumizi.

**Mazrui alisema wizara yake itaweka mashine za kisasa katika hospitali za Pemba hivi karibuni kupitia fedha za serikali na wadau wa maendeleo.**

# Waziri asema hakuna ubaguzi katika utoaji wa adhabu wakiukaji wa sheria

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema adhabu zinazotolewa na mahakama hutolewa kwa mujibu wa sheria na hakuna ubaguzi wowote unaofanywa kwa wanaofanya makosa ya jinai.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Pandani, Prof. Omar Fakih Hamad.

Mwakilishi huyo alitaka kujua kwa nini adhabu za sasa zinawabagua vijana wa kike na wa kiume, kama vile kumlipisha faini kijana wa kiume pindi vijana wawili wakitenda kosa linalofanana.

Waziri huyo alisema sheria ya adhabu Na. 6 ya mwaka 2018, imebainisha makosa mbalimbali ambayo mtu yeyote akitenda makosa hayo, huadhibiwa pale anapotiwa hatiani.

Alisema kwa mujibu wa sheria hizo, adhabu zilizopo hazina ubaguzi wowote wa kijinsia, vijana wa kike na wa kiume wanapewa adhabu zilizo sawa kwa mujibu wa makosa yao na kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya makosa hutendwa na jinsia moja pekee ikiwemo kosa la ubakaji hususan ubakaji wa watoto walio chini ya umri wa miaka 18," alisema.

Alisema kwa mujibu wa kifungu cha 108 (2)(e) cha Sheria ya Adhabu, mtoto wa kike aliye chini ya umri wa miaka 18 hana ridhaa.

Kwa mantiki hiyo, alisema atakayefanya kitendo chochote kinachotengeneza kosa la ubakaji na mtoto huyo anaweza kushtakiwa kwa kosa la kubaka hata kama mtoto wa kike ambaye anaweza kuadhibiwa kwa namna yoyote, kuridhia kuharibiwa heshima yake.

Alisema kwa msingi huo, mtoto wa kike huwa amekosewa na yeye si mkosa katika mazingira hayo.

Pia alisema kutokana na kuwapo kwa malalamiko hayo, wizara yake kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria inaendelea kulifanyia utafiti suala hilo ili kufanya uamuzi mzuri utakaondelea kutunza heshima ya watoto.

"Mheshimiwa Spika, suala la elimu ya malezi mema ya vijana ni wajibu wa taasisi mbalimbali zikiwamo shule, madrasa, wazazi na jamii kwa jumla. Kila mmoja kati ya taasisi hizo, ana wajibu wa kutoa elimu ya malezi kwa vijana wetu," alisema.

Alisema hakuna sheria zinazowabana vijana wa kiume na kuwapendelea vijana wa kike na serikali kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria inaendelea kuzifanyiwa mapitio sheria zote zilizopitwa na wakati na zile ambazo zina dosari kwa lengo la kuzifanyia marekebisho ili ziendane na wakati na kuondosha dosari hizo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI NA. 75 YA MWAKA 2021**
**BAINA YA**
**PUMA ENERGY TANZANIA LTD………………..MDAI**
**DHIDI YA**
**YACOUB MOHAMED KIDULA……………….MDAIWA**

**KWA:**
**YACOUB MOHAMED KIDULA**
**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 17.03.2022 saa 3.00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako maandishi.
**ANGALIZO: -** Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
***Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/muhuri wa Baraza hili leo tarehe 21 ya mwezi wa Februari, 2022.***

---

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD & COURT BROKER**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

KWA IDHINI TULOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO DODOMA MJINI TUTAFANYA MNADA WA HADHARA SIKU YA JUMAMOSI 05/03/2022 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA NYUMBA MOJA ILIYOKO NDACHI BLOCK B' NO. 43 KESI NAMBA 67/2020 MALI YA WANANDOA, FELISTA THADEI MMASI NA CASTELO P. CHAMI.PIA TUTAUZA KIWANJA KILICHOPO NZUGUNI MACHIMBO BLOCK AC' BAADA YA KUSHINDWA KULIPA DENI ALILOKUWA ANADAIWA NA JABIRI NCHEMBA KESI NO. 135/2020, MALI YA HENELY MUHAYO,

**KWA MAWASILIANO TUPIGIE NO. 0713913150 AU 0712643014**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DEOGRATIUS P. MOMBEKI. Anatagaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.903 CDK aina ya TOYOTA LAND CRUSER. yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake Taarifa ya polisi. KAH/RB/78/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

Jazzy Mwanjala Mwandele Anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji tv king Bajaii namba MC972 CCY Model TVS king Mwaka 2018 MBE/MBE/ RB/66845/2022

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA TARAKA NAMBA: 113….2020**

**MDAI: MARTHA SHAYO**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: BRYCESON MCHARO**

**Kwa: BRYCESON MCHARO**

**Ombi la mdai: MARTHA SHAYO**

**Madai ya :Mgawanyo wa mali**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikiliwa mnamo tarehe 08 mwezi 03 mwaka 2022 saa8:30 asubuhi.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama itathibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa Shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 14 mwezi 02 mwaka 2022.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ………..TANGA**

**Kituo cha….. MJINI TANGA…. Mkoa… TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi…………27…………2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: IBRAHIMU WAZIRI SIMBA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: ZUBERI ZUBERI JARIFE**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslai yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 06/03/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa leo 10/02/2022**

HAKIMU
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO TANGA MJINI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ………..TANGA**

**Kituo cha….. MJINI TANGA…. Mkoa… TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi…………37…………2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: MOHAMED HASANI MOHAMED**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: RIKO OMARI RIKO**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslai yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15/03/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa leo 22/02/2022**

HAKIMU
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO TANGA MJINI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE & ADMINISTRATION CAUSE NO. 24 OF 2022**

**In the matter of the estate of the late SALVATORY MAJULA MAPESA**

**And**

**In the matter of the application for letters of administration by JESCA SALVATORY MAJULA and WILLIAM KAITIRA.**

**GENERAL CITATION**

**(Made under Rule 75 of Probate rules, cap 352 R.E 2002)**

All PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above - named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above - named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 16th Day of MARCH,2022

**Dated at Dodoma this 15th Day of February,2022**

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TIZIHWA FRANCIS KAZAGATA** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari (toyota voxy) yenye namba usajili **T 309 CRH** (CHASSIS NUMBER **1A2EAA86495)** yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0763607568. MOR /MOR/RB/63234/2022**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 18 OF 2022**

**In the matter of the estate of the late of the late EMMANUEL CLEMENCE MAKASSY**

**and**

**In the matter of application for letters of administration by ANGELINA ANDERSON MTINYA**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 11/03/2022.

Dated at Dodoma this 18/02/2022

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

HASSAN HALIFA NJENGA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Mitsubishi Canter yenye namba za usajili T332 ATS. Chassis No. FE638E522891, Engine No.4D35E80515. yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya polisi DOD/DOD/RB/71447/2022.

---

## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**IVAN PETER KINGU** Anatangaza kupotelewa kwa ofa ya kiwanja Plot no. **6 Block J LD** kata ya Kihonda Mtaa wa Modeco B, Mali ya Marehemu Petro Aron Kingu yeyote atakae iona atoe Taarifa kituo cha Polisi au piga simu namba **0658-011178. MOR /MOR/RB/75936/2022.**

---

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rais Putin atuma vikosi maeneo yaliyojitenga naye

**Moscow,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladimir Putin ametambua maeneo ya waasi ya Donetsk na Luhansk, ambayo yamejitenga Mashariki mwa Ukraine, kama mataifa huru na hivyo kumaliza mazungumzo ya amani.

Jamhuri za watu zilizojitangaza za Donetsk na Luhansk, ni nyumbani mwa waasi wanaoungwa mkono na Russia, ambao wamekuwa wakipigana na vikosi vya Ukraine tangu 2014.

Wanajeshi wa Russia wameagizwa kufanya kile kinachoitwa 'kazi za kulinda amani' katika mikoa yote miwili.

Rais wa Ukraine, aliishutumu Russia kwa kukiuka mamlaka yake kimakusudi. Katika hotuba yake kupitia televisheni usiku kwa taifa, Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky alisema anataka amani, huku akitangaza kwamba haogopi na nchi yake haitatoa chochote kwa mtu yeyote.

**Russia imeibiwa wakati wa kuanguka kwa Umoja wa Kisovieti (USSR) mwaka 1991, akiishutumu Ukraine kwamba ni koloni la Marekani, linaloendeshwa na serikali ya vibaraka.**

"Kyiv sasa inahitaji hatua madhubuti ya msaada kutoka kwa washirika wake wa kimataifa. "Ni muhimu sana kuona sasa rafiki na mshirika wetu wa kweli ni nani na ni nani ataendelea kutisha, Shirikisho la Urusi kwa maneno tu," aliongeza.

Mataifa yenye nguvu ya Magharibi yanahofia baada ya Rais Putin kutambua maeneo yanayodhibitiwa na waasi na kufungua njia kwa wanajeshi wa Russia, kuingia rasmi Mashariki mwa Ukraine.

Katika miaka ya hivi karibuni, pasi za kusafiria za Russia, zimetolewa kwa idadi kubwa ya watu huko Donetsk na Luhansk na washirika wa Magharibi wanahofia Russia, kuhamisha vitengo vya kijeshi kwa kisingizio cha kulinda raia wake.

Akizungumza katika hotuba ya saa moja, mara baada ya tangazo la Jumatatu wiki hii, Rais Putin alisema Ukraine ya kisasa iliundwa na Russia ya Usovieti, akiitaja nchi hiyo ni ardhi ya Russia ya kale.

Alisema Russia imeibiwa wakati wa kuanguka kwa Umoja wa Kisovieti (USSR) mwaka 1991, akiishutumu Ukraine kwamba ni koloni la Marekani, linaloendeshwa na serikali ya vibaraka.

Pia, Putin, alidai kwamba watu walikuwa wakiteseka chini ya uongozi wake wa sasa na kuyataja maandamano ya mwaka 2014 ambayo yalimwondoa kiongozi wa Ukraine, anayeunga mkono Russia, kama mapinduzi. **BBC**



Familia wakisafiri jana, kutoka eneo la waasi linaloiunga mkono Russia, mjini Stanytsia mkoa wa Luhanska, nchini Ukraine. Eneo hilo ndilo pekee ambalo huwa wazi kila siku kwa ajili ya shughuli hizo, watu kadhaa wamekumbwa na hofu ya vita kutokana na mgogoro baina ya nchi hizo. **PICHA: AFP**

## 'Polisi marufuku kupata ujauzito'

**Lagos,** NIGERIA

MAHAKAMA Kuu Nigeria, imeungana na uamuzi wa kikosi cha polisi kumfuta kazi ofisa wa polisi wa kike ambaye alipata ujauzito nje ya ndoa mwaka jana.

Jaji Inyang Ekwo, amesema hakuona sababu ya kutosha kuvuruga nidhamu ya jeshi.

"Mtu yeyote anayejiunga na jeshi, lazima azingatie kanuni za jeshi au asijiunge na jeshi kwani sio lazima," aliongeza.

Kesi hiyo iliwasilishwa mahakamani na Chama cha Wanasheria Nigeria, baada ya kufutwa kazi kwa ofisa ambaye hajaolewa ambaye alipata ujauzito Januari mwaka jana.

"Maofisa wa polisi wa kiume na maofisa wa polisi waliooa katika Jeshi la Polisi la Nigeria, hawabaguliwi, kuwekewa vikwazo, kuonewa na kudhalilishwa," alisema. **BBC**

## Colombia yahalalisha utoaji mimba

**Bogota,** COLOMBIA

COLOMBIA, imekuwa nchi ya karibuni huko Latin Amerika kutoa fursa ya utoaji mimba, wakati mahakama ya kikatiba ya taifa hilo, ikipiga kura ya kuhalalisha utaratibu wa utoaji mimba hadi wiki ya 24 ya ujauzito.

Uamuzi wa mahakama yenye majaji tisa, haukufikia matarajio ya makundi ambayo yalikuwa yakishinikiza utoaji mimba kuharamishwa kabisa.

Hata hivyo ilielezewa kwamba, tukio la kihistoria na mashirika ya kutetea haki za wanawake ambayo yanakadiria wanawake 800,000 wanatoa mimba kwa siri nchini humo kila mwaka.

Kabla ya uamuzi huo, Colombia iliruhusu utoaji mimba iwapo maisha ya mwanamke yalikuwa hatarini, au mtoto aliye tumboni alikuwa na kasoro ama ujauzito uliotokana na ubakaji. **VOA**

# Uingereza yaondoa masharti ya Uviko-19

**LONDON,** UINGEREZA

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson ametangaza jana, kumalizika kwa masharti yote ya ndani ya Uviko-19 .

Akizungumza mbele ya bunge, Johnson, alisema taifa bado litawahimiza wale wanaopima virusi au wanaopata dalili, kukaa nyumbani, angalau hadi Aprili Mosi, mwaka huu, wakati serikali ikiwahimiza watu waliokutwa na maambukizi au dalili kujikinga kibinafsi.

Pia, nchi hiyo imesema itaacha kulipia upimaji wa Uviko-19.

Johnson alitangaza kuondolewa kwa masharti hayo huku akimtakia kila la kheri, Malkia Elizabeth II, afya njema, baada ya kupimwa na kukutwa na maambukizi wiki iliyopita.

Waziri Mkuu, alisema majibu ya Malkia juu ya kirusi hicho ni ukumbusho kwamba janga hilo bado halijaisha.

Wanasayansi pamoja na wanasiasa wengine wa upinzani wanaonya kwamba, kusitisha upimaji na ufuatiliaji wote wa ugonjwa huo, kutadhoofisha uwezo wa kufuatilia ugonjwa na maambukizi yoyote mapya. **VOA**

## Mlipuko wauwa 59 mgodini

**GBOMBLORA,** BURKINA FASO

MLIPUKO mkubwa umetokea karibu na mgodi wa dhahabu, Kusini mwa nchi ya Burkina Faso na kuua watu 59 na kujeruhi wengine zaidi ya 100.

Shirika la Utangazaji la Burkina Faso (RTB), limesema takwimu hizo zimechapishwa na mamlaka ya mkoa, baada ya tukio hilo lililotokea juzi katika kijiji cha Gbomblora.

Mlipuko huo unashukiwa kusababishwa na kemikali inayotumiwa kusafisha dhahabu, ambayo ilikuwa ikihifadhiwa kwenye eneo la tukio.

Sansan Kambou, ambaye alikuwapo wakati mlipuko huo ukitokea, aliliambia shirika la habari la Associated Press (AP), miili ya watu ilitapakaa kila mahali na ilikuwa ni hali ya kutisha. Sekta ya uchimbaji wa dhahabu, inakua haraka, nchi hiyo ikishika nafasi ya tano Afrika, kwa uuzaji wa madini hayo. Watu zaidi ya milioni 1.5 wanaajiriwa katika sekta hiyo ambayo mwaka 2019, iliingiza kiasi cha dola bilioni mbili. **DW**

HABARI MICHEZO

# KMKM YAKIRI MBIO UBINGWA LIGI KUU Z'BAR BADO NGUMU

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar iliyoingia raundi ya 19, vinara KMKM wamekiri mlima bado ni mrefu kwao katika mbio za kutwaa ubingwa huo msimu huu.

KMKM ipo kileleni ikiwa na alama 42 baada ya kushinda michezo 12, sare sita na kupoteza mechi moja tu hadi sasa kwenye ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.

Vinara hao wanafukuziwa kwa karibu na timu ya Malindi yenye pointi 36 sawa na KVZ huku Machomane ikiburuza mkia kwenye ligi hiyo yenye timu 16, baada ya kuvuna pointi tisa tu katika mechi 19 ilizocheza hadi sasa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa KMKM, Ame Msimu, alisema licha ya kuanza vizuri katika mzunguko huu na kuendelea na matumaini yao ya kutwaa taji la Ligi Kuu Zanzibar, bado mechi zilizobaki zinazidi kuwa ngumu kutokana na kila timu kujiimarisha zaidi.

"Tunaendelea kufanya vizuri, lakini pia ligi inazidi kuwa ngumu, sisi ndio tunaongoza ligi kwa muda mrefu, lakini ndio tunapata wakati mgumu, tunaposhuka dimbani kwa kuwa kila timu inatukamia kuhakikisha inapata alama tatu," alisema.

Mzunguko wa 20 wa ligi hiyo utaendelea Ijumaa wiki hii ambapo Mafunzo itashuka dimbani dhidi ya Selem View katika mchezo utakaopigwa Uwanja wa Amaan majira ya saa kumi alasiri.

Jumla ya timu nne zitashuka daraja msimu huu huku idadi kama hiyo zikipanda Ligi Kuu; ambapo mbili zitatoka Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja na mbili Kanda ya Pemba.

NAPITA...




Kiungo wa Azam FC, Ibrahim Ajibu akiambaa na mpira huku Ramadhani Redondo wa Biashara United akijiandaa kumkabili kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza jana na kumalizika kwa wenyeji kushinda 2-0. **PICHA: AZAM**

## Gariatano apania kumchapa Mpoland

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi nchini, Ismail Gariatano, amesema yupo katika maandalizi makubwa ya pambano la kimataifa lisilo la ubingwa dhidi ya Kamil Laszcyk raia wa Poland.

Pambano hilo la uzani wa Kg 66 ambalo litakuwa la raundi nane, linatarajiwa kufanyika Machi 11, mwaka huu nchini Poland.

Akizungumza na gazeti hili jana, Gariatano alisema anaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya kujiimarisha zaidi katika pambano hilo ambalo atakuwa ugenini kwa mara ya kwanza tangu aingie kwenye tasnia hiyo.

"Mwaka huu nahitaji kufanya vizuri katika mapambano yangu ikiwamo hili la Machi 4, nje ya nchi, nihakikishe napata ushindi ili kujitangaza na kuupa heshima mchezo wa ngumi kwa kuipeperusha vema bendera ya Tanzania," alisema Gariatano.

Gariatano anaenda katika pambano hilo akiwa na kumbukumbu ya kumchapa Mmalawi Denis Mwale kwa pointi za majaji wote pambano lililofanyika mwaka jana katika Ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

## Gekul ageukia usajili UWAWATA

**Na Shufaa Lyimo**

NAIBU Waziri wa Habari Sanaa na Michezo, Pauline Gekul amewataka wasanii wanawake hapa nchini kutumia vizuri vipaji vyao ili waweze kutimiza malengo yao, huku akiwahimiza kuvaa nguo zenye maadili zinazolinda utu wa mwanamke.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana na Chama cha Umoja Wasanii Wanawake nchini (UWAWATA), alisema kwa sasa serikali ikishirikiana na wizara yake itahakikisha inakuwa bega kwa bega na wasanii katika kazi zao.

"Mama Samia Suluhu Hassan ametuagiza tukae pamoja na wasanii ili tuweze kusikiliza changamoto mlizokuwa nazo, lakini pia akikisheni mnapata usajili wa chama chenu.

"Kama mpaka sasa hamjafanikiwa kusajili chama chenu, leo mtaondoka hapa mkiwa tayari mmepata usajili," alisema.

# *COSOTA yafunguka tuhuma ya mirabaha*

**Na Saada Akida**

TAASISI ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), imetoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizotolewa na Taasisi ya Creative Industry Network Tanzania (CNIT), ikiwamo kutoridhishwa na namna mgao wa mirabaha ulivyofanywa pamoja na ukusanywaji wake.

Hatua hiyo imetokana na CNIT kuandika barua kwa COSOTA juu ya tuhuma za masuala ya mirabaha iliyotolewa Januari 28, mwaka huu katika Ukumbi wa Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam ambapo iligawa mirabaha yenye thamani ya Sh. 312, 290, 259 kwa wasanii 1,123 kwa kazi za wasanii wa muziki 5,924 zilizokusanywa kuanzia Julai hadi Novemba 2021 na katika mirabaha iliyotolewa na vituo saba vya redio.

Mirabaha hiyo ilikusanywa kati ya Januari 2019 na Juni 2022, lakini CNIT wakidai ugawaji wa mirabaha hiyo ulitolewa Januari 2022 na Cosota hawakutaja kiasi cha mirabaha kilichokusanywa kati ya mwaka 2019 na 2021.

CNIT pia ilidai kuwa utoaji wa mirabaha hiyo haikuzingatia leja ya kumbukumbu na kukosekana kwa uwazi wa Cosota kutoelewe-ka wadau wa taasisi hiyo kwa kuwasilisha taarifa za hesabu zake, (kuwa wazi katika ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha).

Kuchangia mfuko mkuu wa sanaa na utamaduni na kwamba hakuna bodi ya uongozi wa Cosota tangu mwaka 2008 na maamuzi kutolewa na menejimenti bila bodi.

Akijibu tuhuma hizo jana, Mkurungenzi Mtendaji wa COSOTA, Doren Sinare, alisema mirabaha hiyo ilitolewa kwa sheria za nchi, kanuni na sheria mbalimbali za kimataifa na miongozo yake.

"Mirabaha ile ilitolewa kwa sheria zilizopo hapa nchini, hivyo wadau wanapojadili suala hili wawe wamejiridisha kusoma, kuuliza na kuelewa," alisema.

Doren alieleza kuwa mirabaha hiyo ilitolewa kwa kuzingatia haki mbili ambazo ni maonyesho ya umma na utangazaji ambapo vyanzo hivyo vilipatikana kwa makusanyo ambayo ni hoteli, baa, kumbi za sherehe na vituo vya redio.

"Mirabaha ilikusanywa kati ya Januari 29, 2019 hadi Juni mwaka huu, tangazo la ugawaji wa mirabaha lilitolewa," alisema.

Aidha, Doren alitoa wito kwa wasanii kujisajili COSOTA kwa ajili kupata manufaa ya kazi wanazozifanya ili kuepusha migogoro, na kwamba pia taasisi hiyo itaendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mirabaha kwa kufanya kazi na wadau katika kuboresha sheria na mfumo wa hakimiliki kwa ujumla.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO AGOMBEWA

REAL Madrid watachuana na Manchester United katika kumnasa kocha wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino. (***Mail***)

### SILVA AITAMANI MADRID

KIUNGO wa kati wa Manchester City na Ureno, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 27, ana ndoto ya kuhamia Real Madrid. (***CalcioMercato***)

### RODGERS ANAUNGWA MKONO

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers anaungwa mkono na bodi ya klabu hiyo licha ya mwenendo mbaya timu hiyo. (***Telegraph***)

### BOWEN ATAKIWA LIVER

LIVERPOOL "wana nia ya dhati" kumsajili mshambuliaji wa England, Jarrod Bowen mwenye umri wa miaka 25, kutoka West Ham. (***NipeSport***)

### JESUS ATAKIWA INTER

INTER Milan wanamfuatilia mshambuliaji wa Manchester City na Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 24. (***CalcioMercato***)

### KILMAN AWINDWA CHELSEA

CHELSEA wanavutiwa na mlinzi wa Wolves, Muingereza Max Kilman mwenye umri wa miaka 24. (***Talksport***)

### DAVID AGOMBEWA ULAYA

KLABU za Arsenal, Newcastle, Borussia Dortmund na Inter Milan zinamuwania mshambuliaji wa Lille na Canada, Jonathan David mwenye umri wa miaka 22. (***TuttoMercatoWeb***).

### GOMEZ ANUKIA VILLA

KLABU ya Aston Villa imemfanya mlinzi wa Liverpool na England, Joe Gomez mwenye umri wa miaka 24 kuwa lengo lao kuu msimu wa majira ya joto. (***Football Insider***)

### MBAPPE AOTA MBAWA LIVER

LIVERPOOL wapo nje ya mbio za kumnunua mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, kutoka Paris St-Germain. (***Sport***)

### SPURS YAMSUBIRI KANE

KLABU ya Tottenham Hotspur itasubiri kuanza mazungumzo na mshambuliaji wa Uingereza, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, kuhusu mkataba mpya. (***Athletic***)

### DE GEA KUBAKI UNITED

GOLIKIPA wa Manchester United na Hispania, David De Gea mwenye umri wa miaka 31, amesema yuko tayari kusaini mkataba mpya na klabu hiyo. (***Independent***)

### SHELVEY KUJIFUNGA NEWCASTLE

KIUNGO wa kati wa England, Jonjo Shelvey mwenye umri wa miaka 29, na mlinzi wa Uswizi, Fabian Schar mwenye miaka 30, wako mbioni kusaini mkataba mpya kule Newcastle. (***Telegraph***)

### KEAN KAIKATAA SUNDERLAND

ROY Keane mwenye umri wa miaka 50, alikataa nafasi ya kuwa kocha wa timu ya Sunderland kwa sababu walimpa mkataba wa miezi sita tu na alitaka zaidi. (***Sun***)

### NILES KUTOSWA ROMA

AS Roma haitampa mkataba wa kudumu kiungo wa kati Muingereza Ainsley Maitland-Niles anayecheza kwa mkopo kutoka Arsenal kwa sababu hajafanya vizuri kwenye Serie A. (***Calciomercato, via Mirror***).

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR: NATAKA KWENDA KUCHEZA SOKA MAREKANI

●●● Sijui kama nitacheza tena Brazil, nina mashaka na hilo, ningependa kwenda...

**PARIS,** UFARANSA

MSHAMBULIAJI wa timu ya Taifa ya Brazili na Klabu ya Paris Saint Germain, Neymar amesema angependa kwenda kucheza soka nchini Marekani kwenye Ligi ya Major League Soccer angalau kwa msimu mmoja kabla ya kutundika daluga.

Neymar kwa sasa yuko na mkataba na klabu ya Paris saint Germain ambao unaisha Juni 2025, ikiwa klabu yake ya sasa haitahitaji tena kumuongezea mkataba basi anaweza kutimkia MLS.

Katika mahojiano yake na Jarida la France Football alisema kuwa anavutiwa zaidi kucheza Marekani kuliko nchini mwake Brazil.

> **"Sijui kama nitacheza tena Brazil, nina mashaka na hilo, ningependa kucheza Marekani," alisema Neymar**

"Ningependa kucheza pale angalau hata kwa msimu mmoja, kwanza kabisa wana msimu mfupi, kwahiyo ningekuwa na miezi mitatu ya likizo."

Mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona alisema hajapanga ni wapi ambapo atatundika daluga, lakini alifunguka kuwa atacheza hadi mwishoni mwa mkataba wake pale PSG.

"Nataniana na marafiki zangu kwamba nitastaafu nikiwa na miaka 32, lakini ni utani, sijui, kiukweli, nitacheza mpaka akili yangu itakapochoka, ikiwa akili yangu iko sawa na mwili uko vizuri, nadhani nina miaka michache ya kucheza, lakini afya ya akili ni kitu muhimu sana."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 961,

MECHI KALI
ATLETICO MADRID
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 2.45
X | 3.15
2 | 3.00

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TUCHEL AMKINGIA KIFUA LUKAKU




**LONDON,** England

KOCHA wa Klabu ya Chelsea, Thomas Tuchel hakufurahishwa na kitendo cha watu kucheka kutokana na rekodi ya mshambuliaji wake, Romelu Lukaku ya kugusa mpira mara saba tu kwenye mchezo aliocheza dakika 90.


Lukaku aliweka rekodi hiyo katika mchezo dhidi ya Crystal Palace kwenye Ligi Kuu siku ya Jumamosi ambapo Chelsea walifanikiwa kuibuka na ushindi mwembamba wa bao 1-0.

Tuchel alipoulizwa atamsaidiaje mshambuliaji huyo ili aweze kugusa mpira mara nyingi alijibu;

"Takwimu zipo pale na zinazungumza lugha fulani, hakujihusisha sana mchezoni, muda mwingine inatokea hii kwa washambuliaji, ikiwa watakuwa hawajiamini.

"Si ambacho tunataka au Lukaku anataka, lakini si muda wa kumcheka na kumtania, japo yeye yupo kwenye wakati mzuri, lakini sisi tutamlinda."

Chelsea jana Jumanne ilicheza na Lille kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora.



# De Gea: Naweza kustaafia United

**MANCHESTER,** England

GOLIKIPA namba moja wa Manchester United, David de Gea amesema kwamba, anaweza kumalizia muda uliosalia kwenye soka lake pale Manchester United.

De Gea ambaye alikuwa akiichezea Atletico Madrid kabla ya kujiunga na Man United mwaka 2011, anatarajia kukabiliana na klabu yake hiyo ya zamani leo Jumatano katika usiku wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora katika Uwanja wa Wanda Metropolitano kwa mara ya kwanza tangu aondoke miaka 10 iliyopita.

Kwa mujibu wa takwimu, [De] Gea anashika namba mbili k[wa] kuzuia mabao mengi nyuma [ya] Kepa Arrizabalaga kwenye [m]chuano yote kwa magolikipa [wa] Ligi Kuu England.

"Ukweli ni kwamba nilizali[wa] Madrid, lakini mwisho wa si[ku] ni jiji tu," aliiambia UEFA.

"Sasa najihisi kama ninatok[a] Manchester, najihisi kama ye[ye] te anayetokea Manchester s[e]emu unapopendwa ulipoka[ri]bishwa kama nyumbani kwak[o].

"Sijioni nikiondoka Manch[es]ter United, nipo hapa kwa m[u]aka najua chochote kinawe[za] kutokea kwenye maisha lak[ini] sioni nikiondoka."

## HABARI MICHEZO

# ,840,460

# JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/02/22 | 18:00 | Brighton vs Aston Villa | 2.32 | 3.25 | 3.10 |
| 02. 26/02/22 | 18:00 | Brentford vs Newcastle | 2.41 | 3.25 | 2.95 |
| 03. 26/02/22 | 18:00 | Peterborough vs Hull City | 2.54 | 3.12 | 2.73 |
| 04. 26/02/22 | 18:00 | Millwall vs Sheffield Utd | 2.85 | 3.20 | 2.40 |
| 05. 26/02/22 | 18:00 | Birmingham vs Huddersfield | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 06. 26/02/22 | 19:00 | Sivasspor vs Besiktas | 2.56 | 3.05 | 2.81 |
| 07. 26/02/22 | 20:30 | Oostende vs St Truiden | 2.47 | 3.40 | 2.66 |
| 08. 26/02/22 | 22:45 | Sassuolo vs Fiorentina | 2.75 | 3.44 | 2.47 |
| 09. 27/02/22 | 14:15 | AZ Alkmaar vs Feyenoord | 2.52 | 3.50 | 2.52 |
| 10. 27/02/22 | 15:30 | Hamburger SV vs Werder Bremen | 2.43 | 3.44 | 2.65 |
| 11. 27/02/22 | 16:00 | Alanyaspor vs Konyaspor | 2.45 | 3.16 | 2.86 |
| 12. 27/02/22 | 17:00 | Angers vs Lens | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 13. 27/02/22 | 17:00 | Metz vs Nantes | 2.78 | 3.13 | 2.59 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 23/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 4001 | Mtibwa Sugar vs Young Africans | 6.77 | 3.19 | 1.57 |
| 16:00 | 4120 | Eastern Company SC vs Al Masry Club | 8.47 | 4.53 | 1.36 |
| 16:45 | 2150 | Persebaya Surabaya vs Arema | 3.14 | 3.24 | 2.12 |
| 18:30 | 1604 | Ismaily SC vs El Gouna | 1.63 | 3.55 | 5.52 |
| 19:00 | 4851 | Aris Salonica vs Atromitos | 1.50 | 4.04 | 6.30 |
| 20:00 | 5249 | Aquila 1902 Montevarchi vs Fermana FC | 2.31 | 3.06 | 3.21 |
| 20:30 | 1213 | Lecce vs Cittadella | 1.78 | 3.44 | 4.42 |
| 20:30 | 1551 | Frosinone vs Reggina | 1.70 | 3.48 | 4.91 |
| 20:30 | 2894 | Brescia vs Ascoli | 1.89 | 3.30 | 4.04 |
| 20:30 | 3600 | Ionikos Nikea FC vs Apollon Smyrnis | 1.94 | 3.21 | 4.05 |
| 20:30 | 4513 | Crotone vs Cosenza | 1.93 | 3.24 | 3.93 |
| 20:30 | 5889 | Benevento vs Como | 1.78 | 3.43 | 4.41 |
| 20:45 | 2511 | KAA Gent vs RFC Seraing | 1.28 | 5.80 | 9.40 |
| 21:00 | 4292 | CD Fas U20 vs CD Chalatenango U20 | 1.81 | 3.86 | 3.48 |
| 21:00 | 4403 | Pfeddersheim vs Wormatia Worms | 11.00 | 7.00 | 1.21 |
| 21:00 | 5790 | ETSV Weiche vs St.Pauli II | 1.59 | 3.77 | 4.83 |
| 21:30 | 1453 | FV Dudenhofen vs Hertha Wiesbach | 2.11 | 4.04 | 2.65 |
| 21:30 | 2069 | SV Deutz 05 vs Wesseling-Urfeld | 1.84 | 4.14 | 3.18 |
| 21:30 | 3033 | SV Rodinghausen vs Preussen Munster | 4.23 | 3.75 | 1.67 |
| 21:30 | 3356 | FC Hurth vs Bergisch Gladbach | 7.50 | 5.77 | 1.26 |
| 21:30 | 3626 | UD Biescas vs SD Borja | 2.85 | 3.23 | 2.28 |
| 21:30 | 4597 | VfL Vichttal vs Bor. Freialdenhoven | 2.75 | 4.10 | 2.21 |
| 21:30 | 4666 | Wegberg-Beeck vs Fortuna Koln | 5.77 | 4.04 | 1.47 |
| 21:30 | 4933 | FC Pesch-Bcv Glesch vs Paffendorf | 2.02 | 4.05 | 2.80 |
| 21:30 | 5464 | Jocoro FC U20 vs CD Luis Angel Firpo U20 | 2.01 | 3.67 | 3.04 |
| 22:00 | 2890 | CD Ursaria vs Colonia Moscardo | 1.26 | 5.02 | 9.08 |
| 22:00 | 3345 | AD Villaviciosa vs ED Moratalaz | 2.65 | 3.18 | 2.45 |
| 22:00 | 4493 | Wydad Casablanca vs Hassania Agadir | 1.37 | 4.16 | 7.55 |
| 22:00 | 4549 | CD Manacor vs CF Soller | 1.45 | 4.15 | 5.98 |
| 22:15 | 4490 | AD Complutense Alcala vs AD Torrejon CF | 4.00 | 3.60 | 1.89 |
| 22:30 | 3493 | Trival Valderas A. vs Carabanchel | 1.56 | 4.10 | 5.60 |
| 22:30 | 4650 | CD Tarancon vs CD Huracan De Balazote | 2.00 | 3.50 | 3.65 |
| 22:30 | 5279 | Burnley vs Tottenham | 4.51 | 3.65 | 1.77 |
| 22:30 | 5990 | Watford vs Crystal Palace | 3.15 | 3.15 | 2.35 |
| 22:45 | 1568 | Huddersfield vs Cardiff | 2.21 | 3.19 | 3.19 |
| 22:45 | 3163 | Dundee FC vs St Mirren | 2.70 | 3.15 | 2.70 |
| 22:45 | 3255 | Derby vs Millwall | 2.59 | 2.98 | 2.79 |
| 22:45 | 3956 | QPR vs Blackpool | 1.94 | 3.33 | 3.77 |
| 22:45 | 4164 | Sheffield Utd vs Blackburn | 1.84 | 3.48 | 4.01 |
| 22:45 | 4717 | Stoke City vs Luton Town | 2.09 | 3.28 | 3.38 |
| 22:45 | 5522 | Fulham vs Peterborough | 1.16 | 6.88 | 13.76 |
| 22:45 | 5920 | Liverpool vs Leeds | 1.15 | 8.22 | 14.04 |
| 23:00 | 1061 | Trento Calcio 1921 vs Sudtirol | 6.80 | 3.85 | 1.53 |
| 23:00 | 1177 | Imolese Calcio vs Cesena | 3.65 | 3.35 | 2.06 |
| 23:00 | 2865 | Gubbio vs AC Reggiana | 3.55 | 3.45 | 2.06 |
| 23:00 | 3270 | Benfica vs Ajax | 4.10 | 3.85 | 1.80 |
| 23:00 | 3452 | AD Cariari Pococi vs AD Barrio Mexico | 3.36 | 3.51 | 1.93 |
| 23:00 | 4517 | Atletico Madrid vs Manchester Utd | 2.45 | 3.15 | 3.00 |
| 23:00 | 5634 | Vis Pesaro vs Pescara Calcio | 3.07 | 3.17 | 2.34 |
| 23:00 | 5686 | Louletano vs Moncarapachense | 2.31 | 3.25 | 3.15 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# LUSAJO AZIDI KUWA HATARI NYAVUNI, AKIKATAA KIATU

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA aliyeibuka kuwa hatari nchini Tanzania kwa misimu ya hivi karibuni, Reliants Lusajo wa Namungo, amefikisha mabao 10 baada ya mechi za mzunguko wa kwanza, akiongoza kwenye orodha ya wanaowania Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu msimu huu, huku mwenyewe akisema ana malengo tofauti mbio za kuwania ufungaji bora.

**Juzi, Lusajo alipachika bao moja kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, Namungo ikiiadabisha Mbeya City kwa mabao 2-0 wakati lingine likifungwa na Lucas Kikoti.**

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo, kinara huyo wa mabao katika mechi 15 za mzunguko wa kwanza kwa timu yake, amesema kuwa lengo lake wala si ufungaji bora, badala yake anafunga ili timu yake ipate ushindi.

"Mimi nafunga tu, sishindani na mtu na wala nini, nafunga mabao ili kuiwezesha timu yangu kupata ushindi na kuweza kukaa vizuri kwenye msimamo wa ligi. Nimefunga mabao haya kutokana na ushirikiano mkubwa ninaoupata kutoka kwa wachezaji wenzangu, na wala sifikirii ufungaji bora," alisema Lusajo.

Beki wa Mbeya City, Mpoki Mwakinyuke, amemsifu Lusajo kwa kusema kuwa ni straika hatari kiasi kwamba ukimuachia nafasi, anaitumia.

"Mimi na wenzangu tulijua kuwa ni mchezaji hatari kwetu, tukamuwekea mikakati, lakini nafasi moja aliyoipata kwa sisi kufanya makosa akaitumia, ni straika mzuri sana kwa sasa," alisema nahodha huyo wa Mbeya City, baada ya timu yake kupoteza.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Jamhuri Kihwelo 'Julio', alisema kuwa lengo lao ni kutwaa ubingwa msimu huu na wala si vinginevyo.

"Ubingwa si wa mtu, hata sisi tunaweza kuchukua, tunataka ubingwa, ila kama hatukufanikiwa, basi hata nafasi ya pili au ya tatu," alisema Julio.

Namungo imekwea hadi nafasi ya nne, ikiwa na pointi 23 wakati Mbeya City ikisimama kwenye nafasi ya tano kwa pointi hizo hizo 23, hii ikitokana na kutofautiana mabao ya kufunga na kufungwa.





# TFF yashukia waamuzi Ligi Kuu

**Na Shufaa Lyimo**

MAKAMU wa Rais wa Pili wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Steven Mguto, amewataka waamuzi nchini kufuata kanuni na sheria za soka ili kuchezesha kwa haki na kumaliza kelele nyingi ambazo zimekuwa zikielekezwa kwao.

Mguto aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifunga semina ya waamuzi wa mikoa ya siku tatu iliyofanyika katika Uwanja wa Benjamini Mkapa huku akiweka wazi kuwa kwa sasa wanasubiri kama serikali itafunga teknolojia ya video ya kumsaidia mwamuzi uwanjani (VAR), ili kuondoa makosa hayo ya waamuzi.

"Ninaomba muende mkafuate kanuni na taratibu za mpira ili tuweze kuendeleza soka letu hapa nchini," alisema Mguto.

Mguto alisema kelele za waamuzi haziwezi kumalizika mpaka hapo VAR zitakapofungwa katika viwanja hapa nchini, lakini wanapaswa kuongeza umakini kwa kufuata kanuni na sheria.

Hata hivyo, Mguto alisema Ligi Kuu ya NBC msimu huu imekuwa ngumu kutokana na maandalizi yaliyofanywa na kila timu ikihitaji kupata matokeo, hivyo akawataka waamuzi kuongeza umakini ili kupunguza malalamiko.

# Michezo

Jumatano Februari 23, 2022
Nipashe



Neymar: Nataka kucheza Marekani UKURASA 21

TUPO TAYARI...



Wachezaji wa Yanga wakipozi katika picha baada ya mazoezi, timu hiyo itashuka Uwanja wa Manungu Complex leo kuivaa Mtibwa Sugar kwenye mechi ya kiporo ya Ligi Kuu Bara. **PICHA: MAKTABA**

## Simba kamili leo Morocco

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Simba, watawasili nchini Morocco leo wakitokea Istanbul, Uturuki tayari kwa maandalizi ya mechi ya tatu ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya RS Berkane.

Simba ambayo Jumapili iliyopita ilipata sare ya bao 1-1 dhidi ya Union Sportive Gendarmerie Nationale (USGN) ya Niger, Jumapili wiki hii itashuka uwanjani mjini Berkane kuvaana na RS Berkane iliyotoka kuchapwa mabao 3-1 ugenini dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast.

Baada ya mechi hiyo dhidi ya USGN, Simba ambayo ilianza michuano hiyo kwa kuichapa Asec Mimosas mabao 3-1, ilikwea pipa Jumatatu na kulala jijini Istanbul na leo inatarajiwa kutua jijini Casablanca, Morocco ambapo itaweka kambi ya siku nne kabla ya kuelekea mjini Berkane kwa mechi hiyo.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Meneja Habari wa Simba, Ahmed Ally, alisema wachezaji wote wapo fiti baada ya kupata mapumziko mafupi jijini Istanbul na leo majira ya saa tano wataanza safari kuelekea Morocco.

"Tulifika salama hapa Istanbul, leo (jana) tumepumzika na kesho (leo) saa tano asubuhi tutaanza safari ya kuelekea Morocco.

"Baada ya kufika jijini Casablanca, tutaweka kambi ya siku nne kabla ya kwenda Berkane tayari kwa mchezo wetu wa tatu wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya RS Berkane utakaopigwa Jumapili wiki hii," alisema Ahemed.

Simba inaongoza msimamo wa Kundi D ikiwa na pointi nne ikifuatiwa na Asec Mimosas na RS Berkane zenye alama tatu kila moja huku USGN ikiburuza mkia kwa pointi yake moja. Baada ya mechi hiyo Simba itarejea Dar es Salaam kuisubiri RS Berkane kwenye mechi ya marudiano itakayopigwa Jumapili ya Machi 6, mwaka huu kabla ya kukwea pipa kwenda Ivory Coast kurudiana na Asec Mimosas.

# Yanga, Mtibwa vita kali

### Yasaka rekodi mbili kali Manungu leo, Deo Kanda atajwa kukinukisha kama kocha...

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara Yanga, watashuka kwenye Uwanja wa Manungu Complex baada ya miaka 23, kucheza na wenyeji Mtibwa Sugar, lakini leo ikiwa ni mechi ya kukamilisha mzunguko wa kwanza Tanzania Bara.

**Mara ya mwisho Yanga kucheza mechi kwenye Uwanja huo ilikuwa ni mwaka 1999, ilipocheza dhidi ya Mtibwa Sugar na kutoka sare ya bao 1-1.**

Vinara hao wanakwenda kucheza mechi hiyo leo, baada ya watani zao wa jadi kufanya hivyo, Januari 22, mwaka huu na kulazimishwa suluhu, hivyo wataingia na tahadhari zote kuhakikisha hawasimamishwi azma yao ya kuusaka ubingwa

pia watataka kuweka rekodi ya kupata ushindi katika uwanja huo kwa mara ya kwanza.

Iwapo itashinda au kutoka sare, Yanga pia itaweka rekodi ya kucheza mzunguko wote wa kwanza bila kupoteza mechi yoyote msimu huu.

Ofisa Habari wa klabu hiyo Hassan Bumbuli amesema kikosi chao kimewasili salama mjini Morogoro, wachezaji wakiwa kwenye hali nzuri, lakini akithibitisha wachezaji sita kuukosa mchezo huo.

"Utakuwa mchezo mzuri, tumejipanga kushinda, ingawa tutawakosa baadhi ya wachezaji ambao ni majeruhi. Tutawakosa Yacouba Songne, Jesus Moloko, Abdallah Shaibu 'Ninja', Dickson Job, Kibwana Shomari na Chrispin Ngushi ambao hawajasafiri kabisa kuja Morogoro," alisema.

Msemaji wa klabu ya Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru amesema mechi itakuwa nzuri, kwani na wao wamejipanga vema kuikabili Yanga ambao wanaongoza ligi.

Alisema huenda timu hiyo leo ikamchezesha kwa mara ya kwanza aliyekuwa winga wa timu ya Simba na TP Mazembe, Deo Kanda ambaye ameruhusiwa rasmi na Shirikisho la Soka nchini (TFF), kukipiga na timu hiyo.

"Iwapo kocha itampendeza basi Deo Kanda anaweza kucheza mechi hii, ambayo imevuta mashabiki wengi kuja kutazama. Ni mechi kubwa na ngumu, lakini sisi tumejipanga kushinda ili kujiondoa kwenye hali mbaya tuliyonayo," alisema.

Yanga inaongoza Ligi ikiwa na pointi 36, ikicheza mechi 14, ikishinda 11 na sare tatu wakati Mtibwa Sugar ni ya mwisho kasoro mkia, ikikamata nafasi ya 15, ikiwa na pointi 12 kwa mechi 14 ilizocheza, ikiicha Prisons inayoburuza mkia ikiwa na pointi 11.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >